SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**RIPOTI MAALUMU**

**Wajane** wajuzi wa kuogelea walamba mamilioni baharini

UKURASA 4




UKURASA 9

Nipashe Jumapili
Jumapili Desemba 25, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581170
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Waraka wa maaskofu waibua mambo nyeti

• **Wagusa** janga dawa za kulevya, ulawiti, haki za kisiasa, malezi kwa watoto... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**RAIS SAMIA ATOA ZAWADI KRISMASI**
RAIS Samia Suluhu ametoa zawadi ya vyakula na mbuzi kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi kwenye vituo vitatu...

UKURASA WA 5
**MANISPAA YAJENGA MADARASA IKITUMIA MAPATO YA NDANI**
HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imeanza kutumia mapato yake ya ndani kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi...

UKURASA WA 15
**NAMNA BORA YA KUPAMBA NYUMBA MSIMU WA SIKUKUU**
MSIMU wa sikukuu umewadia huku kukiwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba, kukiwa kunaonekana kutawala...

## Majaliwa ataja mikoa 11 yenye shida kutokana na wingi mifugo

UKURASA 5



Hoteli ya kulaza mbwa iliyojengwa na mfanyabiashara Oscar Nondo wa jijini Arusha.



## Mfanyabiashara ajenga hoteli ya kulaza mbwa

UKURASA 3

**MICHEZO** FEI TOTO ACHAFUA HEWA YANGA, AZAM UK.24

**KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza katika kikao cha pamoja na Mawaziri wa Kisekta, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mkoa na Wilaya za Morogoro cha kujadili changamoto za usimamizi wa ardhi ndani ya mkoa huo, kwenye ukumbi wa Magadu katika Manispaa ya Morogoro jana. **PICHA: PMO**

# Waraka wa maaskofu kwa serikali, wananchi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Makanisa ya Kikristo Mkoa wa Arusha (UKAMA), Askofu Dk. Stanley Hotay ameiomba serikali kuruhusu Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) kwenda kwenye makanisa kutoa elimu ya madhara ya dawa hizo ili kuokoa vijana wanaoathirika zaidi na dawa hizo.

Akitoa salamu za sikukuu ya Krismasi jana jijini Arusha kwenye ibada ya umoja huo, Askofu Dk. Hotay alisema wimbi kubwa la vijana linaangamia kwa dawa hizo na kila kundi linalaumu kundi lingine.

"Tunasherehekea sikukuu hii huku maadili yetu yakiwa yameporomoka na wengi wetu tumetoka kwenye kuwarudisha kundini vijana wetu, tumebaki kurushiana lawama, na wengine tukiwaita vijana wa toyo, hakuna toyo iliyojaa watoto, hawa ni watoto wetu, tusimame kuwarudisha kwenye maadili yetu," alionya.

Alisema hali ni mbaya sana nchini kuliko watu wanavyofikiri, vijana wengi wamefika hatua ya kujidunga sindano na baadhi ya wakubwa wapo nyuma yao. Hata hivyo, hakuwataja wakubwa aliowalenga.

Alisema baadhi yao wamefika hatua hata ya kuleta vurugu kwenye misiba ya wenzao pale wanapofariki dunia na kuzua taharuki kwenye jamii na hata kanisani.

"Kanisa hatuwezi kukaa pembeni, lazima tuwasimamie vijana wetu hawa, tutafakari tulipokosea ni wapi turudishe vijana wetu kwenye maadili yetu, hawa ni watoto wetu.

"Hawa ni watoto wetu na vijana hawa tumewakodi mara nyingi kutupeleka nyumba za ibada na maeneo mengine hata tulipofika hapa, lakini unaogopa kuwashawishi waingie kusali ndipo waendelee na kazi, tunawaacha waondoke, hebu kila mmoja awajibike ili Mungu atusaidie kuokoa kizazi hiki," alisema.

### HAKI KISIASA

Askofu wa Jimbo Kuu Katoliki Arusha Mhashamu Isaac Amani, akitoa salamu za Krismasi kwa niaba ya UKAMA alisema katika maadhimisho ya sikukuu hiyo, ni vizuri kama taifa kwa nyanja zote za kisiasa, elimu na nyingine zitendewe haki ili kila mmoja afurahie amani, mshikamano na upendo wa kweli.

Alisema upendo, mshikamano na amani umejengwa katika misingi ya haki na sheria na hata kuadhimisha miaka 61 ya uhuru bila machafuko nchini siyo jambo dogo, bali ni kubwa na la kumshukuru Mungu na linapaswa kuwa urithi wa kuufanyia kazi ili vizazi vijavyo waendeleze.

### WAZAZI NA MALEZI

Askofu Amani aliwasihi wazazi kuitambua kuwa heshima ya wazazi ni kuzaa na kulea watoto kwa upendo, hivyo ni vyema wakajifunza kwa kuku wa kienyeji namna wanavyofundisha watoto wao.

"Kuku wa kienyeji baada ya kuangua vifaranga huwalea kwa kukaa karibu nao na kuwandaa kwa maisha halisi ya kutafuta na kufanya kazi kwa bidii.

"Kuku wa kisasa hawafanyi hivyo, hawa kuku wa kienyeji wanawalinda na kuvifundisha mbinu ya kutafuta chakula vifaranga vyao. Huwafundisha kupenda kazi na kutafuta chakula bila kuchoka, lakini sisi leo tunalea watoto wetu kama kuku wa kisasa.

"Wapo baadhi ya wazazi ambao hawataki watoto wao waguswe, sababu wanateseka sana. Sasa kama kuku wanaweza, sisi binadamu tutashindwaje?" Askofu Amani alihoji.

Alisema ulimwengu una shida ya kutosaidiana na kushirikiana kama familia kutokana na kuwapo baadhi ya watoto wengine wakiwa wachanga wanakua wazuri, lakini wakishakua hutelekeza wazazi wao na ndugu zao.

"Emmanuel anawataka msaidiane katika nyanja zote za shida na raha, siyo kufarakana, tutumie maadhimisho ya sikukuu hii kurudi kwenye mstari," alisema.

Alisisitiza umuhimu wa familia kuunganisha nguvu kwa kupendana na kusaidiana, huku akiwaomba kuzaa matunda ya heri na baraka na ya upatanisho ya kutendeana mema kama familia ya Nazareth ilivyokuwa ya umoja na upatanisho.

Alisema maadhimisho ya sikukuu ya Krismasi siyo kwa ajili ya kula vizuri, kupamba na kupeana zawadi bali Mungu anataka afanye maskani kwa wanadamu wapate amani ya kweli na si maigizo na wakue kiimani na kuondokana na mabaya.

Pia aliomba umoja huu udumishwe na kurithisha vizazi vijavyo, ili waendelee kuudumisha kwa kuheshimu utu wa kila mtu bila kujali mila na desturi zilizopo.

### ULAWITI

Askofu Amani pia alikemea vitendo vya unajisi na ulawiti wa watoto na udhalilishaji wa watu wenye ulemavu unaofanywa na binadamu na kushika kasi kwa sasa.

"Vitendo hivi vinafanywa na sisi binadamu, hakuna mbwa wala fisi anayebaka au kulawiti binadamu, ila ni sisi wenyewe.

"Kupitia sikukuu hii ya Emmanuel, anatupa ujumbe kama jamii tufikirie upya kuhusu mabaya haya na kuachana nayo," alisema.

Alisema kuwa kibaya zaidi, vitendo hivyo hufanywa na watu walio karibu na familia kama vile ukatili kwa watoto unaofanywa na jirani, ndugu, jamii na jamaa.

### RUSHWA NGONO

Askofu Amani pia alisema matendo ya rushwa ya ngono inayodaiwa kwa mtu ili apate haki yake, yanapaswa kukataliwa na tukomeshwa kwa kuwa ni kinyume cha ubinadamu.

Aliwahimiza wazazi na walezi kusimamia malezi yenye uadilifu na kumgeukia Mungu, huku wakishika njia iliyonyooka na kuepuka kumpa Mungu kisogo.

### RC ARUSHA

Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongela alipongeza UKAMA na Baraza la Maridhiano linalounganisha madhehebu yote na viongozi wa kimila kwa kuwa wamekuwa chachu ya kudumisha amani mkoani hapa.

Alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na makanisa mbalimbali katika kusaidia jamii kwenye nyanja za elimu, afya, mawasiliano, miundombinu na nyingine nyingi, hivyo pale penye uhitaji wa mkono wa serikali, wasisite kueleza ili washirikiane pamoja kisukuma maendeleo.

"Lakini ninashukuru leo (jana) hapa kwa maombi ya kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan, nchi na viongozi wengine wa umma na jami mliyoomba. Ninawaomba endeleeni kuombea nchi yetu ili amani yetu iendelee kudumu," alisema.

# Rais Samia atoa zawadi Krismasi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

RAIS Samia Suluhu ametoa zawadi ya vyakula na mbuzi kwa ajili ya kusherehekea sikukuu ya Krismasi kwenye vituo vitatu vya makao ya watoto vilivyoko maeneo mbalimbali ya Jiji la Arusha.

Vituo vilivyokabidhiwa zawadi hiyo ni Joy of God chenye watoto 24, UmuAisha (16) na Kindeness (45).

Zawadi hizo zilikabidhiwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela kwa niaba ya Rais Samia, kiongozi huyo wa mkoa akisema kuwa Rais ametoa zawadi hizo ikiwa ni ishara ya upendo kwa watoto wanaoishi kwenye vituo hivyo.

Alisema Rais ametoa zawadi hizo ili watoto hao washerehekee Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya.

Zawadi zilizokabidhiwa zinajumuisha biskuti maboksi saba, mchele kilo 200, unga wa ngano kilo 200, mafuta lita 90 na sukari kilo 100.

Mkoa wa Arusha una jumla ya makao 91 yenye watoto 2,567. Kati yao, wa kike ni 1,291 na wa kiume ni 1,276.

Mmoja wa walezi wa watoto hao, Mohamed Ramadhani kutoka UmuAisha, alimshukuru Rais kwa niaba ya wenzake kwa kutoa msaada huo kwa watoto wenye uhitaji.



Shekhe Mkuu wa Jumuiya ya Shia Ithna'ashariyyah Tanzania (TIC) Hemed Jalala, akimkabidhi kadi ya kumtakia krismasi na kheri ya mwaka mpya, Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Dk.Alex Malasusa, hafla iliyofanyika makao makuu ya kanisa hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mfanyabiashara ajenga hoteli ya kulaza mbwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

DUNIA ina mambo! Ndicho unachoweza kusema baada ya Mfanyabiashara, Oscar Nondo wa jijini Arusha kujenga hoteli ya kisasa iliyomgharimu Sh. milioni 80 kwa ajili ya kulaza mbwa wake.

Makazi hayo ya mbwa ambayo hayakutegemewa na wengi kwenye Jiji la Arusha ambalo ni kitovu cha utalii nchini, yamejengwa eneo la Kwa Morombo jijini.

Akizugumza na Nipashe jana nyumbani kwake, Nondo alisema ameamua kujenga hoteli hiyo ya kisasa kama makazi ya mbwa wake kwa kuwa watu wengi wanaofuga mbwa, wanajenga vibanda visivyo na hadhi kwa ajili ya kuwalaza wanyama hao, jambo ambalo siyo sahihi.

"Mbwa wanahitaji kulala mahali pazuri na kula vizuri kama tunavyokula sisi binadamu, hivyo nimeamua kuwajengea 'Lodge' hii ili nao walale mahali pazuri," alisema.

Mfanyabiashara huyo alibainisha kuwa mbwa anaowafuga nyumbani kwake Kwa Morombo, anawachukua kutok Poland, ambao ni aina ya Shepherd na wengine walipo kwa wingi wametoka Afrika Kusini. "Mbwa wanahitaji mafunzo kama tunavyotunza watoto wetu na kila siku lazima kuamka kumjulia hali ili kama anaumwa unaita daktari mara moja anakuja kumtibu," alisema.

Mfanyabiashara huyo alisema kuwa kwa upande wa chakula anawapa nyama ya kuku mara tatu kwa wiki na nyama ya ng'ombe mara tatu kwa wiki kulingana na aina ya mbwa, akifafanua kuwa baadhi hula nyama mbichi na wengine lazima wachemshiwe.

Alibainisha kuwa kwenye nyumba hiyo aliyowajengea mbwa wake, kuna vyumba 10 vyenye uwezo wa kulaza mbwa wawili.

"Lakini nimeanza kutoa huduma ya kulaza mbwa wengine wa watu wanaosafiri au kubanwa kazini kwa gharama ya Sh. 70,000 kwa wiki na wapo wengi wenye uhitaji huu," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo ameona ipo haja ya kuongeza Lodge nyingine kwa ajili ya kutoa huduma nzuri kwa mbwa kwa kuwa wengi huteseka wanapoachwa ovyo mtaani tofauti na wanapoachwa hapo kwake kwa kuwa hupatiwa huduma ya kuogeshwa, kula vizuri na kulala mahali pazuri.

Kutokana na utajiri kwenye biashara hiyo, aliwataka vijana wenzake nchini, kubuni miradi ya kuwaingizia kipato kwa kuwa fursa zipo na waache kutegemea serikali pekee, bali waajiri, akisisitiza "serikali haiwezi kuwapa kazi vijana wote". Mbwa wanaofugwa zaidi nchini kwa ajili ya ulinzi ni aina ya Golden Retriever, Rot Wailers, St Bernard, German shepherd na Caucasian Ovcharka.

Wanaofuga wanyama hao kwa minajili ya ulinzi, huwalea kwa kuzingatia vigezo kadha wa kadha ili waibuke bora katika kulinda. Hata hivyo, aina mbili ya mbwa, German shepherd na Caucasian Ovcharka na Caucasian Shepherd au Caucasian Mountain, ndiyo maarufu katika shughuli za ulinzi.

# Halmashauri yajizatiti kupokea wanafunzi

**Na Friday Simbaya,** MUFINDI

HALMASHAURI ya Mji Mafinga wilayani Mufindi mkoani Iringa imesema iko tayari kuwapokea watoto 2,703 waliofaulu Mtihani wa Darasa la VII.

Kwenye halmashauri hiyo, asilimia 95.5 (wavulana 1,354 wasichana 1,349) ya watahiniwa wa mtihani huo walifaulu.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa madarasa 10 kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima Dendego jana, alisema watahiniwa wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 wamepangiwa shule. Alifafanua kuwa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2022, jumla ya shule za msingi 37 za serikali zilikuwa na watahiniwa 2,831. Kati yao, wavulana walikuwa 1,416 na wasichana walikuwa 1,415.

Alisema Halmashauri ya Mji Mafinga wilayani Mufindi mkoani Iringa ilipokea fedha kiasi cha Sh. milioni 200 toka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa ambavyo ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 100 na katika mabano ni idadi ya vyumba vilivyojengwa kwenye shule za sekondari Luganga (2), Isalavanu (2), Upendo (3), Bumilayinga (2) na Ihongole (1). "Jumla ya watahiniwa 2,703 walifaulu mtihani sawa na asilimia 95.5, wataanza elimu ya sekondari mwakani baada ya madarasa yao kukamilika kwa asilimia 100," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Halima aliipongeza Halmashauri ya Mji Mafinga kwa kukamilisha mradi wa ujenzi wa madarasa kwenye shule za sekondari ili kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka 2023.

"Nimefurahishwa na utekelezaji wa ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa uliokamilika kwa asilimia 100, lengo likiwa ni kuhakikisha wanafunzi wote waliofaulu wanajiunga na kidato cha kwanza hawakosi nafasi," alisema Halima.

Aliwataka wanafunzi kutumia miundombinu hiyo iliyoboreshwa kwa ajili ya kusoma zaidi na si vinginevyo.

Halima pia aliwataka wazazi wa watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, kuhakikisha watoto wao wanaripoti shuleni Januari mwakani na kuanza masomo yao haraka.

Halmashauri ya Mji Mafinga ina jumla ya shule za sekondari 11 zinazomilikiwa na serikali zinazopatikana kwenye kata tisa.

# Waziri ataka utatuzi kero urasimishaji ardhi

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete ameagiza Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam kuitisha miamala ya wananchi wa kata ya kivule wasiopatiwa hati katika urasimishaji makazi holela ili watatuliwe changamoto katika kazi hiyo.

Ridhiwani alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kivule, Manispaa ya Ilala alipokwenda kutoa hati kupitia mkakati wa Wizara ya Ardhi wa kuwapelekea wananchi hatimiliki za ardhi kwenye maeneo yao.

"Kwa kuwa wananchi waliorasimishiwa makazi yao waliacha namba zao za simu, basi kamishna itisha miamala ya wale waliolipa na kuwaelekeza ni kitu gani cha kufanya ili waweze kupata hati," aliagiza.

Katika mkutano huo, wananchi wa Kata ya Kivule walimueleza Naibu Waziri huyo kuwa licha ya kulipa Sh. 160,000, wameshindwa kupatiwa hati na kueleza kuwa kumekuwapo mawasiliano hafifu baina ya wananchi na kamati zinazosimamia kazi hiyo.

Wananchi hao wa Kivule pia walishusha lawama kwa Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) kuwa kinachelewesha kukamilisha urasimishaji kwenye mitaa ya Kivule.

Hata hivyo, Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam, Shukran Kyando alibainisha kuwa Chuo cha Ardhi Morogoro kimefanya kazi kwa zaidi ya asilimia 80 lakini fedha zilizotolewa na wananchi kwa ajili ya kazi hiyo ni asilimia 11 tu.

"Kata ya Kivuke ina mitaa minne na Chuo cha Ardhi Morogoro kimeingia mkataba wa kufanya kazi kwenye mitaa hiyo kwa ajili ya kumalizia kazi ya urasimishaji lakini zipo changamoto mbili, yaani upande wa kampuni na ule wa wananchi kutolipia viwanja zaidi ya 7,000 ambavyo vimeidhinishwa," alisema Kyando.

Naibu Waziri wa Ardhi, Ridhiwani, kupitia mkutano huo alikitaka Chuo cha Ardhi Morogoro kupeleka miamala yote iliyofanyiwa kazi kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dar es Salaam na kusisitiza kuwa taarifa zote zinazokusanywa kuhusiana na kazi ya urasimishaji, mwenye mamlaka nazo ni kamishna na siyo kampuni.

"Kama kuna maeneo yamekwama, basi kampuni ziongee na kamishna ili kujua namna ya kutatua kero ili kwenda mbele na ninaelekeza hadi kufikia tarehe Mosi Februari mwakani, suala la wananchi wa Kivule kuhusiana na urasimishaji makazi tuwe tumemalizana nalo," aliagiza Ridhiwani.

RIPOTI MAALUM

# Wajane wajuzi kuogelea wanavyolamba mamilioni kupitia kilimo cha baharini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR



ZANZIBAR ni visiwa vilivyozungukwa na Bahari ya Hindi na wakazi wake wanaitegemea kwa kiwango kikubwa kuendesha maisha yao.

Licha ya utegemezi huo kwa bahari kujipatia kipato, wengi wao hawajui kuogelea, hasa wanawake.

Lakini kwa wanawake wa Kijiji cha Jambiani kuna utofauti, wengi wao ni wajuzi wa kuogelea kutokana na kujikita katika kilimo cha sponji kinachoendeshwa kwenye kina kirefu cha maji ya bahari.

Sponji ni moja ya mazao ya bahari, ikifanana na dodoki ambalo kwa Zanzibar na Tanzania Bara linatumika kwa kuogea.

Kilimo hicho ni mbadala wa kilimo cha mwani, kikitoa ajira kwa zaidi wakulima 36,000, asilimia 90 wakiwa ni wanawake, kwa mujibu wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi.

Kinakopatikana Kijiji cha Jambiani ni kusini mwa Kisiwa cha Unguja, Km 40 kutoka Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Huko ndiko Nipashe inakutana na wakulima wa sponji, akiwamo Nasiri Hassan Haji (47) anayetamba kuwa na uzoefu wa miaka minane, akifaidi matunda ya kilimo hicho.

Mwanamama Nasiri anasema moja ya masharti ya kilimo hicho ni mkulima kuwa na ujuzi wa kuogelea, kwa sasa kilimo hicho kikifanyika Jambiani pekee kwa Zanzibar.

"Nililima mwani kwa miaka 15 lakini sikuona faida yoyote, baada ya kuanza kulima sponji kuna mabadiliko makubwa, kipato changu kimeongezeka," anasema Nasiri, mama wa watoto wanne.

Nasiri ambaye pia ni Mwenyekiti wa Ushirika wa Wakulima wa Sponji unaojumuisha wanachama 13, wengi wao wakiwa wajane, anasimulia kuwa mara ya kwanza alipoingia kwenye kilimo hicho, jamii ya kijiji hicho ilimshangaa kutokana na uamuzi wake wa kuacha kulima mwani na kulima sponji.

"Hali ilikuwa ngumu na ilifika hatua nikapoteza matumaini kwa sababu kilimo cha sponji kinalimwa kina kirefu cha maji na mimi sikuwa na ujuzi mkubwa wa kuogelea.

"Kutokana na kupata mafunzo mazuri ya kuogelea, sasa ninakimudu vyema kilimo cha sponji. Kwa kweli tulifunzwa vizuri jinsi ya kuogelea na sasa mimi ni mjuzi na ni mwalimu kwa wengine," anatamba Nasiri ambaye ni mjane.

Nasiri anabainisha kuwa wakati akilima mwani, alikuwa anaziona sponji zinazagaa baharini lakini hakuna aliyefahamu umuhimu wake na kama wangelima na kupata fedha nyingi.

"Mwaka 2014, mimi na mwenzangu (Kazija Omar) tuliunganishwa na Taasisi ya Marine Culture ambayo ilitufundisha kulima sponji na kutupatia mafunzo ya kuogelea.

"Sasa kilimo cha sponji ni mkombozi kwetu, kinatuwezesha kutunza familia bila kutegemea msaada wa mume. Ninamiliki nyumba, watoto wangu wanapata milo mitatu kwa siku na wanapata huduma zote muhimu yakiwamo mahitaji ya shuleni.

"Kutokana na mafanikio hayo, hasa nilipojenga nyumba, sasa wanawake wengi wameshajikita kwenye kilimo cha sponji," Nasiri anafafanua.

Mkulima mwingine wa sponji, Zulfa Abdallah (31) anabainisha kuwa kama ilivyokuwa kwa Nasiri, naye alikuwa mkulima wa mwani lakini aliachana na kilimo hicho kutokana na kutoiona tija.

Kama ilivyo kwa mwenyekiti wao Nasiri, Zulfa anasema kilimo cha sponji kimemsaidia kubadili maisha na kuongeza kipato chake.

"Nimenunua kiwanja na vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kujenga nyumba ya kudumu na watoto wangu watatu wanakwenda shuleni bila usumbufu," anasema Zulfa.

Hata hivyo, mkulima huyo anataja vikwazo katika kilimo hicho kuwa vinajumuisha ugumu uliopo katika upatikanaji wa mbegu, vifaa na utaalamu wa kukabiliana na maradhi.

"Upatikanaji wa mbegu ni wa shida kwa sababu watu wanaolima sponji wameongezeka. Msimu uliopita wa baridi tulipoteza sponji nyingi kutokana na kuharibika, bado hatujui tatizo lilikuwa nini," anasema Zulfa ambaye ni Katibu wa Ushirika huo.

Hindu Simai Rajab (29), mkulima mwingine wa sponji, anasifu utajiri uliopo kwenye kilimo hicho, akilaumu walichelewa kukigundua.

"Kwa mwezi ninaweza kupata hadi Sh. 300,000, fedha ambazo sikuwahi kumiliki wakati ninalima mwani," anasema Hindu na kubainisha kilimo cha sponji kimemsaidia kutunza familia na kupata mahitaji mengine bila kutegemea mume.

Hindu anaeleza kuwa soko la sponji liko zaidi kwenye sekta ya utalii, akiwa na ufafanuzi wa bei ya soko la bidhaa zao, akitamka:

"Sponji moja ndogo tunauza hadi dola 15, hivyo soko likiwa zuri tunaweza kufanya biashara kubwa kwa sababu tuna sponji za kutosha ambazo zinasubiri soko."

Ili kufaidika zaidi na kilimo hicho, Hindu na wanaushirika wenzake wanaiomba serikali kuwatafutia soko la uhakika kama ilivyo kwa mazao ya mwani na karafuu.

**WALIMU WAO**

Ali Masoud Ali, Meneja Miradi wa Taasisi ya Marine Culture iliyoko Jambiani anajivunia kilimo cha sponji kilivyobadilisha maisha ya wanawake wa eneo hilo.



Mkulima wa Sponji, Nasiri Hassan Haji akiwa kazini kwenye Bahari ya Hindi hivi karibuni. **PICHA ZOTE: RAHMA SULEIMAN**

"Baada ya kilimo cha mwani kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, tulifikiria kuja na mbadala wa kilimo hicho ambacho ni sponji kwa kuwakusanya wanawake na kuwapa elimu ambayo sasa wanaitumia vizuri na inawanufaisha," anasema.

Ali anaendelea kubainisha kuwa malengo ya taasisi yao ni kutanua kilimo hicho kwa wakazi wa vijiji vingine vya mwambao wa Bahari ya Hindi na kutafuta soko la sponji nje ya nchi.

Pia anasema wanajivunia kuwawezesha wanawake kuwa wajuzi wa kuogelea ambapo kwa sasa wana uwezo wa kuogelea hadi mita 12 na kuwa chini ya maji ya bahari hata kwa saa tatu.

"Tuliwafunza kilimo hiki wanawake wajane kwa sababu wanapitia changamoto mbalimbali katika kupata mahitaji kulinganishwa na walio kwenye ndoa," anafafanua.

**HATUA SERIKALINI**

Mkurugenzi wa Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Soud Ahmed anasema kilimo hicho mbali ya kuongeza kipato cha wakulima, pia ni rafiki mkubwa wa mazingira ya bahari.

"Kwa sababu sponji inatumika kwa kuogea inaimarisha afya ya ngozi na kuzuia wadudu wanaoshambulia ngozi, pia inaweza kutumika kutengeneza dawa ya kuua malaria na kukabiliana na kansa," anasema.

Bishara Ali Juma, Ofisa Utafiti kutoka Kitengo cha Utafiti wa Mazao ya Bahari, anasema hakuna utafiti uliofanywa kuhusu kilimo hicho kwa Zanzibar, lakini ni kilimo kizuri ambacho kinahitaji kuendelezwa.

"Tunakusudia kufanya utafiti kubaini manufaa makubwa ya kilimo na kama kinaweza kustawi maeneo mengine ukiachia Jambiani," anasema.

Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Suleiman Massoud Makame anasema katika kuendeleza uchumi wa bluu, mikakati ya serikali inajumuisha kuwawezesha wakulima wa mazao ya baharini wakiwamo wakulima wa sponji.

Kwa mujibu wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), nchi za Mediterranean na Caribbean zina wakulima wakubwa wa sponji lakini soko kubwa liko Marekani, Hispania, Japan, Ufaransa na Italia.

FAO inaitaja Tunisia kuwa msafirishaji mkubwa wa sponji duniani na asilimia 90 ya bidhaa hiyo inauzwa Ufaransa ikifuatiwa na Cuba.



Mhitimu wa Shahada ya Sanaa katika Utawala wa Umma, Zulfa Hassan Hussein akipokea cheti cha ushindi wa alama za juu, kutoka kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi katika mahafali ya Chuo Kikuu cha Zanzibar hivi karibuni. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Majaliwa amulika mikoa yenye migogoro kutokana na mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa ameitaja mikoa ya Morogoro, Iringa, Pwani, Lindi, Arusha, Manyara, Kagera, Katavi, Tabora, Tanga na Mwanza kuongoza katika shida za kijamii na kimazingira zinazosababishwa na mifugo.

Amesema mikoa 11 hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi zinazosababishwa na mifugo ikiwamo migogoro ya wakulima na wafugaji, uharibifu wa vyanzo vya maji na misitu iliyohifadhiwa kisheria.

Katika kikao kazi cha viongozi mkoani Morogoro jana, Majaliwa alisema kikao hicho kinachotokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan yanahusu kusimamia kwa karibu sekta ya mifugo ili kutatua kero zilizopo.

"Leo (jana) tunaona changamoto kubwa za wakulima na wafugaji zinazosababisha mauaji, wanakatana mapanga, hata jana (juzi) niliangalia kwenye runinga, nikaona kuna mahali wakulima wanalalamika mifugo imeingia kwenye mashamba yao ya mpunga na kuharibu mazao," alisema.

Majaliwa alisema kutokana na hali hiyo, kila kiongozi anapaswa kuwajibika kwa kusimamia haki, usalama na kutoa elimu elimu kwa jamii ambayo kwa sasa imekuwa na roho ya kikatili.

Majaliwa alisema kutokana na migogoro hiyo ya wakulima na wafugaji, jamii imekuwa na chuki, pia kumekuwa na vitendo vya rushwa miongoni mwa viongozi ambao pia wamekuwa wakichochea migogoro hiyo.

"Polisi wenyewe sasa hivi wameanza kudhibitiwa na wananchi, juzi juzi tu huko Malinyi ama Ulanga, polisi walifungiwa ndani ya nyumba chini ya udhibiti wa wananchi, tukifika hapo hiyo haina tija. "Chombo cha ulinzi na usalama kinadhibitiwa na raia, nini maana ya kuwapo kwake? Kwanini imetokea hiyo? Wananchi wamechoka au sisi viongozi hatuwajibiki?" Majaliwa alihoji.

Alisema Mkuu wa Nchi anapoonyesha kutoridhishwa na maeneo fulani, ni wajibu wa viongozi hao kuweka mpango mkakati wa pamoja wa kudhibiti changamoto za mifugo na kujua nini cha kufanya katika kukabiliana na changamoto hiyo.

Awali akitoa salamu za mkoa, Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa alisema kuwa yeye pamoja na viongozi wenzake wako tayari kupokea na kutekeleza maagizo na maelekezo yote yatakayotolewa na Waziri Mkuu na serikali kwa ujumla.

Alisema ujio wa Waziri Mkuu umeleta faraja kwa viongozi na wananchi wa Mkoa wa Morogoro.

Kikao hicho kiliwahusisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa, wakuu wa wilaya zote za mkoa huo, wenyeviti wa halmashauri, makatibu tawala wa wilaya, wakuu wa taasisi za umma ikiwamo Mamlaka ya Wanyamapori (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), kamati za ulinzi na usalama za wilaya na wakurugenzi kutoka Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Baadhi ya mawaziri walioambatana na Waziri Mkuu ni pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Anjela Kairuki; Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki; Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete na Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde.

# Manispaa yajenga madarasa ikitumia mapato ya ndani

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imeanza kutumia mapato yake ya ndani kwa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi vyumba vya madarasa kwenye shule za msingi ili kumaliza tatizo la upungufu wa madarasa.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Ally Machela alisema jana kuwa utekelezaji huo umeanza kwa kujengwa madarasa 10 yaliyogharimu Sh. milioni 220 zilizotokana na mapato ya ndani.

Alifafanua kuwa ujenzi wa vyumba hivyo ulianza Septemba 4 mwaka huu na kukamilika Septemba 30 mwaka huu, hivyo tayari madarasa hayo yameanza kutumika.

"Tumeshajenga vyumba vya madarasa 10 ambayo kwa sasa yanatumika, fedha hizi ni mapato ya ndani ya bajeti yetu ya mwaka 2022/23, ninatumia nafasi hii kulishukuru Baraza la Madiwani kwa kufanya uamuzi huu," alipongeza.

Alibainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23, Halmashauri ya Manispaa imepanga kujenga vyumba 50 vya madarasa kwenye shule za msingi kupitia fedha za mapato ya ndani.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa madarasa yaliyopo kwenye shule zao za msingi ni 656 ilhali mahitaji ni madarasa 1,539 hadi kufikia Juni mwaka huu.

Meya wa Manispaa hiyo, Pascal Kihanga, alisema manispaa yao inaendelea kukua kwa kasi kwa kuwa miradi mingi imetekelezwa na kuendelea kutekelezwa kupitia fedha za ruzuku na fedha za mapato ya ndani.

# Wahariri waipongeza serikali mabadiliko Sheria ya Habari

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wahariri na wajumbe wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) wamepongeza uamuzi wa serikali kuwasilisha bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016.

Wamesema kitendo cha serikali kuweka hadharani kwamba imepanga kuwasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo kinaonyesha nia ya kuifanyia marekebisho sheria hiyo ambayo kwa miaka kadhaa imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa habari nchini.

Wahariri hao waliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam walipozungumza na waandishi wa habari kuhusu kusudio hilo la serikali.

Wahariri hao walikuwa wakizungumzia kauli ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye aliyoitoa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam wakati akizungumza kwenye Kongamano la Maendeleo ya Sekta ya Habari.

Katika hotuba yake, Nape aliwahakikishia wadau hao wa habari kwamba serikali imedhamiria kuifanyia marekebisho sheria hiyo na katika kudhihirisha hilo katika Bunge la Januari mwakani, serikali inatarajia kuwasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo.

"Niwahakikishie kuwa serikali itafanyia mabadiliko sheria hiyo ya habari kwa wakati na tunatarajia kuwasilisha muswada wakati wa Bunge la Januari mwakani.

"Pamoja na hayo, tuelewe kwamba hakuna maendeleo katika nchi yoyote bila kuwa na waandishi wa habari ndiyo maana tunataka sekta ya habari itumike kuleta maendeleo kwenye sekta zingine nchini," alisema Nape.

Mjumbe wa TEF, Maregesi Paul ambaye pia ni Mhariri Mkuu wa Gazeti la TanzaniaDaima, alisema kauli hiyo ya Nape inatia moyo na inaonyesha ni kwa kiasi gani serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kuikuza tasnia ya habari.

"Binafsi nilifurahia kauli hiyo kwani inaonyesha serikali imedhamiria kuikuza tasnia ya habari kwa vitendo.

"Kwa hiyo, jukumu letu kama TEF na wadau wa habari nchini, ni kuendelea kuionyesha serikali kwamba mabadiliko ya sheria hiyo yaendane na kilichokuwa kikilalamikiwa na waandishi wa habari pamoja na wadau wa habari kwa ujumla," alisema Paul.

Mjumbe wa TEF ambaye ni mmoja wa wahariri katika Gazeti la Mwananchi, William Shao alisema pamoja na kauli nzuri ya Waziri Nape, kinachotakiwa sasa ni wadau wa habari kuhakikisha maoni yao yanatekelezwa kwa asilimia zote kwani huo ndiyo msingi wa malalamiko yetu.

"Serikali imesema ina nia njema na sekta ya habari na ndiyo maana sasa imepanga kuwasilisha bungeni muswada wa mabadiliko ya sheria hiyo ya habari.

"Hiyo ni nia njema, lakini hadi sasa haionyeshi maoni ya wadau yatatekelezwa kama yalivyopendekezwa au yatachukuliwa machache na mengine mengi kutupwa kapuni.

"Kwa hiyo, jambo la msingi ni wadau wa habari kutokaa mbali na serikali bali tuongeze ushawishi serikalini ili maoni yetu yachukuliwe kama yalivyo na hatimaye Tanzania tupate sheria bora itakayokuwa mfano kwa nchi zingine duniani," alisema Shao.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusherehekee Krismasi hii kwa kudumisha amani

**LEO** ni Sikukuu ya Krismasi ambayo Wakristo duniani kote wanaadhimisha kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Mwokozi wao Yesu Kristo zaidi ya miaka 2,000 iliyopita.

Krismasi ni Sikukuu ambayo huvuta hisia za watu wengi wa imani ya Kikristo na wasio wa imani hiyo na baadhi ya watu husafiri kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kuungana na ndugu, jamaa na marafiki kwa ajili ya kuisherehekea. Kwa baadhi ya makabila, ni wakati wa familia kukusanyika katika sehemu wanayotoka na kujadiliana masuala ya familia na kama kuna kasoro miongoni mwao, wanazirekebisha.

Kama ilivyo ada, sikukuu hii husherehekewa kwa namna tofauti na kwa wale wanaofuata ibada, huanza na mkesha ambao ulifanyika jana katika makanisa mbalimbali huku viongozi wa dini, kwa maana ya mapadri, maaskofu na wachungaji wakitoa ujumbe kwa waumini wao namna ya kuenenda maisha yenye kumpendeza Mungu.

Aidha, leo katika makanisa mbalimbali, Wakristo watakusanyika kwa ajili ya ibada zitakazotoa fursa pia kwa viongozi wakuu wa madhehebu hayo, hususan maaskofu, kutoa ujumbe si kwa ajili ya waumini wao tu bali hata kwa jamii nzima kulingana na masuala mbalimbali yaliyoko na yanayotendeka katika jamii. Zaidi, viongozi hao huhimiza amani, haki na watu kuishi kwa kupendana pamoja na kukemea vitendo viovu vinavyojitokeza katika jamii.

Nchini Tanzania na pengine mataifa mbalimbali, kutokana na jamii kuishi kwa amani na upendo na kushirikiana katika masuala ya shida na raha, sikukuu hii hujumuisha hata wale wasio na imani ya Kikristo kama ambavyo hufanyika kwa sikukuu za Kiislamu. Watu wote hukusanyika katika sherehe hasa vyakula bila kubaguana.

Kama wahenga wasemavyo katika msafara wa mamba na kenge wamo, pamoja na maudhui ya Krismasi kuwa ni kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu Kristo kwa watu kwenda kwenye ibada na baada ya hapo watu kukusanyika sehemu waliyoiteua kwa ajili ya kupata vyakula na vinywaji, wako baadhi ya watu ambao hufanya mambo yasiyofaa katika jamii wakati wa Krismasi.

Baadhi ya mambo ambayo watu hao huitia doa sikukuu hii adhimu ni kufanya uasherati na ulevi, uhalifu kama vile ujambazi na wizi. Miongoni mwa watu, wakiwamo Wakristo, hunywa vileo mpaka kupitiliza huku wengine wakiendesha hali wamelewa na hatimaye kusababisha ajali. Wako wengine ambao hupigana na hata kutoana ngeu au kuuana kabisa.

Nyakati za usiku, hufanyika burudani za aina mbalimbali ambazo huambatana na starehe kama vinywaji na wakati mwingine katika maeneo ya burudani hutokea madhara yakiwamo watu kujeruhiana na kutoana uhai. Jambo lingine ni kuwapo kwa disko toto, burudani ambayo huhusisha watoto kupelekwa kwenye kumbi na kucheza muziki.

Ni vyema jamii ikabadilika na kutambua kuwa sikukuu kama Krismasi na zingine za kidini, si kwa ajili ya kufanya maasi na vitendo ambavyo ni kinyume cha maadili ya imani husika.

Kwa mantiki hiyo, katika kusherehekea sikukuu ya Krismasi, ni vyema jamii hasa familia zikatulia na kujadili masuala ya maisha badala ya kufanya mambo ambayo ni chukizo mbele za Mwenyezi Mungu. Krismasi itumike kudumisha upendo na amani miongoni mwa watu huku waumini wa Kikristo wakitambua kuwa kuzaliwa kwa Yesu kristo ni ukombozi kwao na si kufanya vurugu na ukiukwaji wa sheria za nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Jamii isibweteke, ukatili wa kijinsia una madhara mengi

Na Sabato Kasika

**UKATILI** wa kijinsia, unatajwa kuwa na matokeo mabaya kwa manusura, na kwamba madhara yake hudumu katika kipindi chote cha maisha, na yanaweza kuharibu fursa ya mtu kuishi maisha mazuri, yenye afya na yenye mafanikio.

Vilevile inaelezwa kuwa vitendo hivyo vinaathiri wanawake kiafya, kimwili na kisaikolojia, huku athari hizo zikihafifisha uwezo wao kushiriki masuala ya kiuchumi na uwezo wa kuboresha maisha ya familia.

Kwa watoto, vinaathiri ukuaji wa ubongo wao, wanapopatwa au kushuhudia vitendo vya kikatili, na kwamba nafasi yao ya kukua kimwili na kiafya inaathirika, na inawezekana wasifanye vizuri darasani.

Kutokana na athari hizo na nyingine, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa kupinga vitendo hivyo, imekuwa ikifanya kila njia kuhakikisha ukatili usiwe sehemu ya maisha ya kila siku ndani ya jamii.

Imekuwa ikitoa elimu ya kuzuia ukatili katika jamii kwa lengo la ustawi bora wa wanawake na watoto ambao kimsingi ni taifa la kesho, na ndio maana hivi karibuni kulikuwa na timu iliyozunguka mikoani kutoa elimu.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), na Mtandao wa Kupinga na Kupambana na Ukatili wa Kijinsia (MKUKI), walifanya maadhimisho ya kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini.

Kampeni hiyo ilihusisha Msafara wa uanaharakati ambao ulizunguka katika mikoa saba ya Pwani, Morogoro, Singida, Shinyanga, Geita, Mara na Arusha, kwa ajili ya kupaza sauti ya kupinga ukatili wa kijinsia.

Desemba 10 mwaka huu, ilikuwa ni mwisho wa kampeni hiyo, ambayo iliongozwa na kaulimbiu isemayo; 'Kila uhai una thamani, tokomeza mauaji na ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto'.

Ninadhani pamoja na kumalizika kwa kampeni hiyo kusiwe mwisho wa vita dhidi ya vitendo vya ukatili katika jamii, na vita hiyo isiwe ya kusubiri maadhimisho au siku maalum, badala yake iwe ni endelevu.

Vitendo vya ukatili ambavyo vimekuwa vikijitokeza kwenye baadhi ya maeneo nchini, ni pamoja na ukeketaji, vipigo, ubakaji, ulawiti, utelekezwaji wa familia utupwaji wa watoto, rushwa ya ngono na vingine vingi.

Ukiangalia suala la ukeketaji, ni wazi bado kikwazo, kwani siku chache zilizopita tangu kumalizika kwa siku 16 za maadhimisho ya kupinga ukatili wa kijinsia, tayari baadhi ya watoto wamekimbia kwao kukwepa kukeketwa.

Wiki iliyopita, Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, Seleman Bishagazi, alisema kituo chake kimepokea watoto watatu waliokimbia toka kwao maeneo ya Kitunda wakihofia vitendo hivyo.

Kwamba mwezi huu wa Desemba baadhi ya makabila yanayojihusisha na vitendo hivyo, huwa ni ya ukeketaji, na kwamba watoto ambao wamepata elimu kuhusu madhara ya ukeketaji, hukimbia kuukwepa.

Ninadhani kuna haja ya kuongeza kasi ya kutoa elimu badala ya kusubiri maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili ambazo inawezekana zisiwe na matokeo mazuri zaidi kuliko elimu ambayo ingetolewa kila mara.

Mila na desturi potofu ambazo zinaendelea kupewa uzito na baadhi ya jamii, zinaweza kutoweka iwapo kila mmoja wetu ataona umuhimu wa kuachana nazo hasa baada ya kuelimishwa kwa kina.

Aidha, kampeni ya kupinga ukatili wa kijinsia ingekuwa ni ajenda ya kudumu katika vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Mkoa (RCC), Wilaya (DCC), Kata (WDC) na vijiji, lakini pia viongozi wa dini na wazee wa mila washirikishwe.

Si vibaya wadau mbalimbali wakajitokeza kuunga mkono kampeni hizi kwa kuchangia rasilimali fedha, ili wananchi wengi zaidi wafikiwe na kuelimishwa, lakini pia kupatiwa msaada wa kisheria.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA



Pascal Mayala

# Tupendane kwa dhati Krisimasi hii

HERI ya Krismasi. Sikukuu ya mwaka huu imedondokea siku nzuri ya Jumapili. Kwa vile Krismasi ni sikukuu ya Kizungu iliyoletwa Afrika na ujio wa Wamisionari walioleta dini ya Kikiristo Afrika, nimeamua kuwatakia heri ya Sikukuu ya Krismasi kwa kuitumia lugha yake ya asili iliyokuja nayo, yaani Kiingereza. Nasema hivyo kwa sababu kuna vitu ukivitamka kwa lugha yake ya asili, vinanoga zaidi, kupendeza zaidi na kukolea zaidi kuliko ukivitamka kwa lugha ya tafsiri.

Japo Krisimasi ni Sikukuu ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Masiha, Bwana wetu Yesu Kristo, kwa sisi Wakristo, inaadhimishwa dunia nzima na watu wa dini zote na mataifa yote. Hata nchi za Kiislamu, kwa kitu kinachoitwa 'Christmas Spirit is Giving', yaani dhima ya Krismasi ni kutoa, kujitoa, kukipelekea zawadi kichanga kilichozaliwa leo.

Lakini kwenye maisha yetu, si lazima kuwapo kichanga kilichozaliwa leo, hivyo hiyo 'roho' ni ya kutoa kwa waliotuzunguka, ukianzia kwenye familia yako, majirani ndipo twende kwa ndugu, jamaa na marafiki hadi kwa wazazi wetu vijijini. Ni sikukuu ya kutoa na si sikukuu ya kupokea.

Tena ukitoa, toa kwa wote bila kujali ni wa dini gani maana Krismasi ni sikukuu ya wote. Hata kwenye dini ya Kiislamu, wanamtambua Masiya, Bwana wetu Yesu Kristo, kama Nabii Issa Bin Maryam. Ukisoma sifa za huyo Nabii Issa bin Maryam, utakubaliana na mimi mtu huyo ni Yesu Kristo lakini kwa vile kila dini iko huru kuamini imani yake, kuna dini zinamkubali Yesu ndiye Nabii Issa, hivyo kuzaliwa kwake kunasherehekewa dunia nzima. Ni sikukuu ya wote.

Hata simulizi za mwanzo wa ulimwengu kwa dini kuu mbili za Wakristo na Waislamu, sote tunakubaliana dunia iliumbwa na Mungu, mwanzo Mungu aliwaumba Adam na Eva (Kikristo) au Adam na Hawa (Kiislamu), hivyo sisi binadamu wote ni watoto wa baba mmoja, Adam. Hata neno mwanadamu au binadamu, maana yake ni Mwana wa Adamu au Bin Adam. Hata sisi nembo yetu ya Taifa yenye mwanamke na mwanamume, Bibi na Bwana, wale ni wazazi wetu, Adam na Hawa.

Kwa dini zote mbili kuu duniani, Wakristo na Waislamu, tunaamini kisa cha Nabii Abraham (Kikristo) Ibrahimu (Kiislamu) na mkewe Sara (Kikristo), Sarai (Kiislamu), waliishi muda mrefu kwenye ndoa yao bila kubahatika kupata mtoto. Baada ya uzee kuwanyemelea na mkewe Sara siku zake kukoma, hivyo kutokuwa na uwezo tena wa kuzaa mtoto, ndipo akamtoa mjakazi wake wa Kimisri, Hajira (Kikristo), Hagir (Kiislamu) kushiriki na mumuwe Ibrahim ili kupata mrithi.

Huyo mjakazi akashika ujauzito, akamzaa mwana wa kwanza wa Ibrahimu akaitwa Ishamel (Kikristu) Ismail (Kiislamu), aliyemzaa na huyo mjakazi wake wa Kimisri. Familia nzima ilifurahi kupata mtoto, baba, mama na mjakazi.

Baadaye kwa muujiza wa Mungu, mke wa Ibrahim, Sara, akiwa mzee wa umri wa miaka 80, alishika ujauzito, na kumzaa mtoto aliyeitwa Isaka (Kikristu), Isihaka (Kiislamu). Ismail ndiye Baba wa Waislamu wote, na Isaka ndiye baba wa Wakristo wote.

Ni katika ukoo huu ndio alikuja kuzaliwa Nabii Musa na ndiye aliyewakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri na ndie aliyepewa Amri Kuu za Mungu ni zile zile amri alizopewa Musa, kupitia Torati, na hata Yesu alipokuja, bado amri za Mungu ni zile zile za Musa. Yesu hakuja kuitengua Torati bali kuikamilisha, hivyo Wakristo na Waislamu ni watoto wa baba mmoja, tusherekee Krismasi pamoja.

Kuna Watanzania wengi wanajiandaa kwa mwaka mzima, ikiwamo kuweka akiba ya fedha za kutumia kula Krismasi. Wanajikuta wanaisherehekea kinyume cha malengo, badala ya kutoa, wao ndio kwanza wanatumia kwa kujipenda, kufanya matumizi makubwa na sherehe, kula, kunywa, kusafiri, kustarehe, kununua vitu na kujipa zawadi badala ya kuwapa zawadi wengine, hasa wahitaji.

Amri kuu kuliko zote ni upendo. Ukimpenda mtu kwa dhati, utamtakia heri, fanaka na mafanikio. Natoa wito kwa sisi Watanzania, tupendane kwa upendo wa dhati. Viongozi pendaneni na wapendeni wenzenu hata wapinzani! Ukiwa na upendo wa dhati toka moyoni mwako, haiwezekani ninyi mkakutana na tena vikao vyenu vingine mkavifanyia hata pale patakatifu petu, lakini mkawazuia wenzenu kufanya mikutano. Tupendane kwa dhati na tusiwatendee wengine hiyana.

Hebu basi kwa wiki hii, waangalie majirani zako waliokuzunguka ni watu wenye hali gani. Wakumbuke wagonjwa walioko hospitalini, wafungwa magezarani, yatima kwenye nyumba za watoto yatima au watu wengine wowote wenye uhitaji. Hebu jitoe uwashike mkono kwa kidogo chochote kitu ili kudumisha "The Christmas Spirit, to give', kwa kujitoa kwa upendo kuwatolea chochote ili na wao pia washerehekee Krismasi.

***Nawatakia Heri ya Krismasi na Mwaka Mpya***

***Pascal Mayalla***
***+255 754 270403***

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



Na Joseph Kulangwa
kulangwasos@gmail.com

# Nakutakieni Noeli njema na mgawo wa maji, umeme!

LEO ni 'Hepi Besi Dei' ya Yesu Kristo, aliyezaliwa zaidi ya miaka 2,000 iliyopita katika mji wa Yerusalemu kwa baba Yosefu na mama Mariamu, kwenye hori la kulia ng'ombe.

Ni siku ambayo wanaiita Krismasi au Noeli. Ni siku ya mapumziko. Wakristo duniani wanaiadhimisha kwa aina tofauti tofauti, kwa ibada na hatimaye karamu au tafrija na michapalo mbalimbali maeneo tofauti tofauti.

Wako waliozaliwa siku moja au siku inayofanana kwa tarehe na hii ya leo ambao utawasikia baadhi wakienda na majina ya Noel au Noela, ingawa sijasikia wanaoitwa Krismasi au Krismasa. Viongozi wetu wa dini wanaweza kutwambia.

Hii siku ingetakiwa kuwa maalumu kwa watoto lakini kwa kuwa watu wazima wanataka kufanya kila kitu, ndiyo sababu wakaamua kuiteka na kuwa yao huku wakiwadanganya watoto kwa kuwanunulia nguo mpya kwa ajili hiyo.

Ni siku ambayo Wakristo wanaiadhimisha kwa ukubwa na uzito wake, ingawa si Wakristo wote wanaotambua kuzaliwa kwa Yesu Kristo siku ya leo, wakidai hakuna anayejua fika na kuthibitisha kuwa ndiyo hasa aliyozaliwa mkombozi wao huyo.

Lakini hata hao wasioamini hivyo, nao wanaingia kwenye mkumbo wa kuisherehekea, wakiungana na wenzao wenye imani hiyo, kumwagilia nyoyo kwenye baa na vilabu vya pombe za kienyeji na kulewa chakari.

Ukiona watu wanamwagilia nyoyo huko kwenye vijiwe vyao, usidhani wote wana furaha kwani wamekamuliwa vilivyo na watoto kwa nguo mpya na vyakula tofauti na vya kila siku. Leo watu wamejikamua na kuna mapilau majumbani.

Si wote walionunulia wanao nguo mpya, wako wenzangu mie pangu pakavu tia mchuzi walioijikusuru na kupata angalau vijigauni, vijishati, vijisuruali, vijifulana na vijikaptura vya mitumba, kwa ajili ya watoto wao.

Ni aghalabu kwa mtoto kutofautisha huu ni mtumba na hii ni nguo mpya kutoka duka la bei, hivyo akishaona ana nguo ambayo tangu azaliwe hajaiona kuitia mwilini mwake, basi hapo naye kamwagilia moyo kiaina yake.

Kwa watu wazima mliovamia sherehe hizi za watoto, leo isiishie kumwagilia nyoyo, bali ni siku ambayo unaweza kumsaidia mwenzio asiyenacho, kama una nguo haikutoshi, basi usiitumie kupigia deki, bali mtafute aendaye uchi mfunike mwili kwa nguo hiyo.

Nawe uliyekula na kusaza, usimwage kilichosalia bali mtafute mwenzio aendaye njaa, ili umsitiri njaa na hivyo kupata nguvu ya kuwaza nini afanye kwa maisha yake, kwa sababu mtu haulizwi kala nini bali kavaa nini, hatatambulika kuwa kala kilichosalia kwako.

Wanasema ukifanya ukarimu huo hata Mungu hukuona na kurudishia ulikopunguza, hiyo ina maana na wale wenye ukwasi basi nao wasisite kusaidia wenye ukata, lakini bila kusahau kutoa sadaka makanisani kwani watoao Neno la Mungu nao ni binadamu wenye mahitaji. Wasisahaulike wote waishio katika mazingira magumu.

Hii ni siku ya kusameheana kwa waliokoseana, lakini pia ni ya kutubu kwa wale walioamua kudhulumu haki za wenzao kwa maslahi binafsi ya Tumbo Street kwani Mungu anakuoneni mnapofanya maskhara na maisha ya wenzenu kwa kuwazibia riziki na kudhulumu haki zao.

Zamani hakukuwa na dhuluma kama hizi za sasa, ambapo mtu anakudhulumu huku akikutazama machoni bila kukuonea aibu, pia watu walikula kwa kiasi si kama sasa wanafakamia mpaka kutisha na hata kusababisha kutafutiwa suluhu.

Oneni sasa mpaka Prof. Mohamed Janabi na wenzake wa Muhimbili, wameamua kuja na maputo ya kuwawekea walaji sana matumboni ili kupunguza ulaji mwingi, unaowasababishia matatizo ya kiafya, kwa kutawaliwa na ulafi usiopimika.

Bila shaka Jeshi la Polisi nalo limeshatoa hadhari kwa waendeshao vyombo vya moto kuacha kufanya hivyo wakiwa wamemwagilia nyoyo hususan leo, ili kuepusha ajali za kijinga, likisema: "Dereva akinaswa amelewa, moja kwa moja mahakamani." Haya sasa kazi kwenu masuka.

Naamini hadhari hii itakuwa kwa vitendo, tofauti na zile zingine dhidi ya bodaboda wasiovaa kofia ngumu na wasiosimama kwenye taa nyekundu, huku pia wakivuka alama za pundamilia barabarani bila kusimama, lakini pia bila kusahau kubeba abiria mishikaki. Jamani eeh Merry and Happy Christmas! Yaani Noeli Njema kwenu bila maji na umeme! Alamsiki!

***Ujumbe kwa watangazaji: Wingi wa mwamba ni miamba si wamba!***

# HABARI PICHANI



Sehemu ya wananchi wa kata ya Kivule, wilaya ya Ilala, wakimsikiliza Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete (hayuko pichani) wakati wa utoaji hati uliotokana na urasimishaji makazi holela katika eneo hilo. **PICHA: MUNIR SHEMWETA.**



Mkurugenzi wa Chuo cha Uuguzi cha Elljerry na kituo cha biashara cha Msekwa Park kilichoko barabara kuu ya Muheza – Amani, mkoani Tanga, Elizabert Chigua, akizungumza na wananchi jana katika uzinduzi wa kituo cha biashara cha Msekwa Park. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**



Wachuuzi wa samaki wakiandaa kitoweo hicho kwa ajili ya kuwauzia wateja wao katika Soko la Samaki la Kimataifa Feri, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA.**



Wakazi wa kijiji cha Magila, Muheza mkoani Tanga, wakiwa katika mkutano katika Shule ya Sekondari ya Magila, juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza, ambaye pia ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akimkabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 14, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Magu, Dk. Maria Kapinga (kulia) kwa ajili ya kusaidia watoto njiti katika Hospitali ya Wilaya ya Magu, juzi hospitalini hapo. **PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Ukurasa 13

**WAWEZA KUTOKA HIVI SIKUKUU YA KRISMASI**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Namna bora ya kupamba nyumba msimu wa sikukuu



2 MAISHA JUMAPILI DESEMBA 25, 2022

MAHAFALI

AHITIMU WA CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR (ZU) WALIOPATA TUZO KWA KUPATA ALAMA ZA JUU WAKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA RAIS WA NZIBAR.

Mhitimu Shahada ya Uhusiano wa Umma, Zulfa Hassan Hussein katika picha za pamoja na Mwalimu Ahmed Ally Abdallah wa somo la 'Organisational Development and Management', pamoja na ndugu na marafiki waliofika kumpongeza katika mahafali ya Chuo




# Urembo wa pete na maana zake

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | L | A | A | N | A |
| | A | | | Y | |
| M | W | A | | U | |
| | A | | I | N | A |
| | M | | | G | |
| S | A | U | M | U | |

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, UGA, SANDA, PENDO, PAGAWA, DANDIA

## TOA TOFAUTI 5



## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

ANGALIA KWA MAKINI KIVULI HIKI, UNAFIKIRI MTU HAYA ANAJIANDAA KWA MCHEZO GANI?



## CHEKA

Alichokifanya daktari

**M**TOTO Suzana akiwa varandani na mama yake akimsaidia kazi za nyumbani. Wakati wakiendelea na kazi Suzana alimuuliza mama yake.

**Suzana:** Mama naomba nikuulize kitu kuhusu bahari

**Mama Suzana:** Sawa niulize tu

**Suzana:** Eti kuna samaki anayeitwa Nguva anafanana na binadamu, tena mrembo kama malaika?

**Mama Suzana:** Hakuna samaki wa aina hiyo

**Suzana:** Kumbe wanatuongopea hakuna samaki Nguva?

**Mama Suzana**: Samaki Nguva yupo lakini hana umbo la binadamu, hayo ni mapokeo na hadithi tu.

============

**SWALI**

Swali; Paa ni jamii ya Mnyama gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Binti anahonga mchumba fedha, anamwacha anaoa mwingine!

***KARIBU tena msomaji wangu tumalizie mwaka 2022 kwa ushindi. Ni mwaka uliosheheni mambo mengi na kila mmoja wetu anajua kile alichopitia mwaka huu, kiwe kizuri au kibaya. Yote hayo ni maisha kwani milima na mabonde havikosekani!***

HERI ya Krismasi. Tushangilie pamoja kumbukizi ya kuzaliwa kwa Masihi wa BWANA zaidi ya miaka 2000 iliyopita. Bado safu hii inaangaza anga la vijana katika uhusiano.

Nilieleza huko nyuma kwamba vijana wengi bado wanahangaika kutafuta wenza wao ili waishi maisha ya ndoa. Wako wanaofanikiwa na wengine bado wanajiuliza maswali mbona hawapenyi.

Kundi hili ndilo nalimulika leo. Wako wengine hufikia hatua wanahonga fedha wanaume ili waolewe nao. Matokeo yake huishia maumivu rohoni.

Baadaye nitatoa mfano wa dada mmoja ambaye kila anayemtaka amoe anamwacha. Na huyo anayemwacha huoa mwanamke mwingine mbele ya macho yake! Ama kweli Maisha Ndivyo Yalivyo.

Katika hali ya kawaida mwanamume ndiye anayeanza kumuongelesha mwanamke kwa habari ya kutaka mahusiano. Ndiye anayeanzisha mada ya mahusiano.

Inapotokea mwanamke ndiye mwanzilishi wa mada, uwezekano wa mwanamume kushtuka ni mkubwa. Atajiuliza, mbona analazimisha nimtake, tena kwa kunirubuni fedha. Kama si rushwa katika mapenzi ni kitu gani?

Katika maandiko ya Mungu, tunaonyeshwa kuwa mwanamume ni kiumbe cha mwanzo. Mungu alimuumba Adamu wa kwanza (mwanamume), kisha baada ya hapo akamuumba mwanamke kuwa msaidizi wa huyu mwanamume.

Ukiona mwanamke anachukua nafasi ya mwanamume, ujue tayari hiyo nyumba ina shida. Siku zote baba ni kiongozi wa familia au kaya.

Hebu sasa msomaji wangu sikia kisa cha dada huyu ambaye umri wake unaenda, lakini bado anasaka mchumba kwa staili ya kuhonga fedha wanaume ili akubalike. Pamoja na mbinu hiyo, bado wanamuacha kwenye taa nyekundu.

Dada huyu anatoka moja ya mikoa ya Kaskazini. Alipata mchumba miaka miwili iliyopita, akawa anamhonga Sh.10,000 kila mara kama kivutio watangaze uchumba.

Kijana akahamaki, akahisi kama ananunuliwa. Walikuwa wanasali kanisa moja, kijana anaamua kukimbilia mikoani. Dada hakukata tamaa.

Akamvamia kijana mwingine pia wa kanisani kwao. Akamshawishi waende akamtambulishe kwa wazazi wake. Dada akagharimia kila kitu nauli na kadhalika, wakaondoka.

Baada ya kurejea Dar, haijulikani kijana aligundua nini huko kwa wakwe watarajiwa. Kimya kimya kijana akaanzisha mchakato wa kusaka mchumba mwingine.

Alipompata akatangaza uchumba madhabahuni. Yule dada akabaki kukodoa macho kwani hakuamini yule mchumba aliyempeleka kwao amebadilisha nia na kumvisha pete mwingine.

Huyu dada hakuishia hapo. Akampata kijana mwingine akamrubuni tena kwa fedha zake. Watu wanaomfahamu kijana huyu, wanaona anampotezea muda kwani anayo malengo yake. Ni kijana anayejitambua na tayari anatafuta namna ya kumkwepa kwani ameshampata ampendaye.

Mpenzi msomaji, naamini sasa umepata picha kuhusu staili ya huyu dada kusaka wachumba kwa kurubuni fedha na nini kinachompata baada ya hapo.

Hakika, kinachomtokea siyo kwa bahati mbaya, ipo nguvu au roho zinazozuia asifanikiwe katika eneo hilo. Ziko roho za mizimu zinawashikilia vijana wengi na kuathiri mahusiano yao. Hii ni silaha kubwa sana inayotumiwa na shetani kuwaunganisha watu na mizimu.

Kuna kitovu chenye nguvu kinachowaunganisha kila mwanadamu kwa mababu zake. Hili nitalichambua vizuri wiki ijayo tukiukaribisha mwaka mpya 2023 kwa neema ya Mungu.

Dada niliyemjadili, yamkini anasumbuliwa na mojawapo ya roho zifuatazo;- Mizimu, kukataliwa na pia mitala (ndoa za wake wengi). Majira kama haya ya mwisho wa mwaka, watu wengi hufunga safari kwenda vijijini kwa kusanyiko la kifamilia au ukoo.

Ni utaraibu wa asili ulioanzishwa na mababu, familia hukaa pamoja huchinja, kula na kunywa. Hukusanyika kukazia viapo na maagano yaliyofanywa na waasisi/mababu zama hizo.

Leo wazee hao hawapo lakini bado mila zinaendelezwa. Matokeo yake vijana wanateswa na asili hiyo katika ndoa, biashara na hata elimu, pasipo wao kujua chanzo. Ni vyema unapokuwa na changamoto, rudi nyuma tafuta chanzo. Utajua kilichofanywa na mababu na kuchukua hatua sahihi, yakiwemo maombi ya nguvu.

Yafaa watu kuwa makini misimu kama hii ya Krismasi, tukwepe miungu, tumtafute sana Mungu. Tukutane wiki ijayo.

***Una kisa? Ujumbe 0715268581.***

***Msomaji wangu, niishie hapa. Wiki ijayo nitakuletea kisa cha kimaisha cha kusisimua ambapo shangazi katika familia fulani alijifungua boga. Je, ilikuwaje na nini kiliendelea? Una maoni au kisa? Tuma ujumbe mfupi 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tusimlaumu Mungu mabadiliko ya tabianchi, chanzo ni sisi

UNAPOSAFIRI kwenda Bwawa la Julius Nyerere kupitia Ngerengere mkoani Morogoro, utaona kazi ya uharibifu wa mazingira ilivyo kubwa, kiasi cha ardhi kubakia yenye vichaka vidogo vidogo.

Ikiwa hujawahi kupita njia hiyo awali unaweza kuona huenda pako hivyo tangu kuumbwa kwa ulimwengu, kumbe ni binadamu wamesababisha hali kuwa ilivyo.

Kuna eneo ukifika unachoona ni moshi mdogo mdogo unaelekea angani huku eneo likiwa na vichaka vidogo vidogo. Hii inaonyesha kiasi gani wananchi wamegeuza misitu kuwa maeneo ya ajira zao.

Huko watu wanakata mkaa kama hawana akili nzuri, kama hawajui kuna kesho kama wanaona hiyo miti waliyokata ikipandwa upya leo kesho inafaa kuvunwa kwa mkaa.

Ukiwa mkoani Dar es Salaam, unaletewa magunia kwa magunia ya mkaa unautumia nyumbani huwezi kujua ni miti kiasi gani imevunwa na sasa ardhi imebaki tupu.

Tunalia kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha mvua kuwa haba na hazipo kabisa, kiasi cha shida ya maji kuongezeka na migogoro kuzidi.

Huko kwenye vijiji makundi ya mifugo yamejaa ambayo inaelezwa ni ya wakubwa fulani ambao wana fedha nyingi kiasi kwamba anaweza kuingiza mifugo kwenye shamba fulani halafu akalipa fedha yoyote ambayo mwenye shamba ametaka.

Maana yake fedha si tatizo kabisa kwao bali mifugo yao ile ishibe ili iendelee kuongezeka. Serikali za vijiji ziko mikononi mwa wafugaji ambao hutembeza fedha kwa kadri ya hali ilivyo.

Pia ukienda kwenye bwawa hilo, hali ni hiyo hiyo kwa eneo la Kisarawe ambalo Mbunge wake ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Suleiman Jafo, nako wananchi wamevuna vya kutosha kiasi cha kuonekana ajira pekee ni uchomaji mkaa.

Malalamiko ya uharibifu wa vyanzo vya maji ni makubwa na hata mikoa 10 itakayochangia maji kwenye bwawa hilo, nako hali si ya kuridhisha. Maana yake ni janga la taifa linalotutaka wote kuona tatizo na kuchukua hatua.

Yako mazoea kwamba wali wa kupikwa kwa mkaa ni mtamu zaidi ambayo yanapaswa kuondolewa ili watu waamini kwenye kutumia nishati ya gesi au umeme kupikia, ni vyema zikapatikana kwa bei rahisi ili kukabili uharibifu.

Viongozi wengi hasa wa maeneo husika wanashindwa kukemea uharibifu wa mazingira kwa sababu ya kuhofia kupoteza wapiga kura, lakini uwapo wa viongozi wajuu kwenye maeneo hayo kunawafanya viongozi wa chini kushindwa kusema jambo maana wataondolewa.

Ndiyo maana Mkuu wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro alisema bayana kwamba hawezi kuondoa mifugo iliyopo humo maana ni mali ya wakubwa, huyu ni mmoja kati ya wengi waliopata ujasiri wa kusema.

Ila naamini wako wakuu wa mikoa na wilaya hawawezi kusema maana juu yao kuna mawaziri na vigogo wengine ambao wana maslahi makubwa juu ya jambo hilo ambalo kimsingi ni maumivu kwa wengi.

Naamini agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuwashughulikia hao 'wakubwa' litafanyiwa kazi na watatajwa hadharani ili wawe mfano kwa jamii. Ikiwa litakwenda kimya kimya itaonekana ni kawaida yetu kusema alafu jambo linaishia hapo.

Uzuri ni kwamba athari za mabadiliko ya tabia nchi ni kwa wote bila kujali ulisababisha au hukusababisha ndio maana shida ya maji ilivyoingia Dar miezi michache iliyopita, ilituumiza sote.

Ni lazima hatua stahili zichukuliwe ili kuokoa mazingira yetu, mazingira yakiharibika hata uhai wa binadamu hautakuwepo,iwe ni ajenda yetu sote vinginevyo maisha yetu yataisha.

Bila kudhibiti matumizi ya mkaa kwa kuhakikisha kuna nishati mbadala hali itaendelea kuwa ngumu na mazingira yataendelea kuteketea ni lazima kuchukua hatua zinazotekelezeka isiwe ni maneno kwenye majukwaa au makaratasi.

Ikiachwa hivi utafika wakati hali ya jangwa itaongezeka kiasi cha wananchi kuingia kwenye vita ya maji na wakati huo haitakuwa ni wakati wa kumuomba Mungu ambaye ametupa akili,utashi na mazingira mazuri ila kwa ujuaji wetu wanadamu tumeharibu kila kitu.

Sipingani na maelekezo ya kumwomba Mungu ili mvua inyeshe lakini tujiulize wanadamu tumefanya nini kutunza alichotupa muumba wetu, kwa nini tumeharibu na tunaendelea kuharibu tena kwa kasi kubwa sana alafu tunarudi madhabahuni kumwomba alete mvua?

**Mungu Ibariki Tanzania**
**Mungu Ibariki Afrika.**

# MAHAFALI



WAHITIMU WA CHUO KIKUU CHA ZANZIBAR (ZU) WALIOPATA TUZO KWA KUPATA ALAMA ZA JUU WAKIWA KATIKA PICHA YA PAMOJA NA RAIS WA ZANZIBAR.













Mhitimu Shahada ya Uhusiano wa Umma, Zulfa Hassan Hussein katika picha za pamoja na Mwalimu Ahmed Ally Abdallah wa somo la 'Organisational Development and Management', pamoja na ndugu na marafiki waliofika kumpongeza katika mahafali ya Chuo kikuu cha Zanzibar hivi karibuni.



# MITINDO

Na Christina Mwakangale



## KINAMAMA WANAWEZA KUTOKA HIVI KWA SIKUKUU YA KRISMASI

LEO ni Sikukuu ya Krismasi. Ni sikukuu ambayo Wakristo duniani wanaadhimisha kuzaliwa kwa Mwokozi Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

Katika maadhimisho hayo, waumini wa Kikristo hufurika makanisani kwa ajili ya ibada ambazo kwa kawaida huanzia na mkesha wa Krismasi. Huwa ni sikukuu muhimu kwa waumini hao. Kutokana na umuhimu huo, baadhi ya watu huona ni afadhali wakose ibada za Jumapili zote za mwaka lakini ibada ya Krismasi si ya kukosa.

Inapokaribia sikukuu hiyo, vichwa vya watu hugonga wakijiuliza watavaa nguo gani katika siku hiyo adhimu ambayo huwa ni mara moja kwa mwaka? Kutokana na mawazo hayo, ndipo watu hubuni au kuwaza ni nguo gani wanaweza kununua wakaonekana 'wametoka' kiaina wakati wa kuadhimisha Krismasi.

Wanamama ndiyo usiseme. Kwa wengi wao, siku hiyo ni muhimu sana, hivyo suala la mavazi kwao ni kipaumbele hasa lile vazi la ibada.

Wakati leo ikiwa ndiyo Krismasi, hii ndiyo mitindo ambayo kinamama wanaweza kuvaa na wakapendeza na siku hiyo ikaisha kwa roho kwatu. Unaweza kuvaa sketi na blauzi ukatoka 'mchicha' au suti ya kitenge.

Kadhalika unaweza kuvaa suti ya vitambaa mchanganyiko wa nguo ya kawaida (spesho) iliyochanganywa na kitenge au gauni ambalo katika mitindo linakuwa gumzo kwa muda mwingi.

Wengine wanaweza kuvaa gauni la kitenge lenye urefu wa kuvuka magoti, vijana wa mjini wanaita gauni la heshima na wakaonekana nadhifu.

Yote kwa yote, Krismasi ndiyo habari ya mjini kwa mitindo hasa kwa kinamama.









UREMBO



# Urembo wa pete na maana zake

KATIKA ulimwengu wa mitindo lazima tukubali kuwa inasaidia kutufundisha na kutupa maujuzi mbalimbali.

Leo kwenye safu hii nakuletea namna ya kuvaa pete vidoleni na maana zake ili kujua aina ya urembo wako unaotumia.

Miaka kadhaa iliyopita ulikuwa ukimuona mtu amevaa pete basi unajua huyu anakaribia kuolewa au ameshaolewa, ila kwa sasa kuvaa pete za urembo zenye nakshi nakshi ni kitu cha kawaida na huvutia vidole vya mtu husika.

Pete hizi zipo tofauti tofauti zingine zinakuwa na herufi za jina la mtu na zingine zinakuwa plain na zipo za vito.

**UNAVAAJE:**

Ukitaka uvae pete hizo basi hakikisha una pete zaidi ya tatu zenye mionekano tofauti, kisha vaa katika vidole vyako.

Pete yenye herufu ya jina vaa kidole cha kati ili kuvutia zaidi.

Kwa pete zingine unaweza kuvaa katika vidole tofauti, mfano ukivaa pete kidole gumba ni ishara ya kuwa na afya njema na mali.

Ukivaa pete kidole cha pili ni ishara ya kuwa kiongozi au mtawala kwenye jamii.

Kidole cha kati ni ishara ya ujasiri na harakati za kutafuta mwenza wa maisha yako.

Pete kidole cha pili kutoka cha mwisho ni cha uchumba au ndoa na kidole cha kati ni urembo.

Kidole cha mwisho kinamaanisha uaminifu, mwenye akili na anayependa familia.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Jinsi ya kupika wali mzuri nazi wa maua wenye kunukia

MSIMU huu wa sikukuu madikodiko ni muhimu jikoni kwako hasa kubadili aina ya mapishi kwa kuongeza nakshi.

Katika safu yetu ya mapishi nitakuelekeza namna ya kupika wali wa maua, ili kubadili kidogo badala ya kupika pilau au wali mweupe na familia yako itafurahia mlo huu.

**Mahitaji**

Mchele, karoti, hoho, hiliki, njegere, kitunguu swaumu, tangawizi, nazi ya kukuna ni nzuri zaidi na chumvi.

Kuna nazi yako vizuri uikamue na uichuje kidogo kiasi cha maji yatakayotosha mchele wako kisha bandika tui jikoni lichemke

Osha njegere, chambua mchele na uoshe, chambua kitunguu saum menya na tangawizi kisha visage kwa pamoja, chota kijiko kimoja kikubwa cha chakula cha mchanganyiko huo na katakata karoti na hoho muundo wa viboksi vidogodogo.



**Jinsi ya kupika**

Bandika sufuria yako jikoni, weka mafuta kiasi kisha kabla hayajapata moto weka njegere hii inazuia njegere kutorukaruka, koroga hadi njegere zibadilike rangi

Kisha weka Karoti endelea kukuroga

Weka mchanganyiko wa tangawizi na kitunguu saumu koroga hapa usichelewe sana maana vitunguu huwa vinawahi kushika chini, weka hiliki kisha mchele.

Koroga hadi vichanganyike haswaaa, kisha weka tui lako la nazi lote ulilochuja kisha weka chumvi koroga na ufunike.

Baada ya muda angalia wali wako kama umekauka ile nazi uliyoweka kisha palilia na weka moto juu na chini kidogo.

Subiri kama dakika 20 angalia kama umeiva weka hoho ulizokwisha zikata hapo awali kisha geuza kidogo na funika tena kwa dakika tano.

Baada ya hapo waweza pakua wali wako ukiwa na harufu nzuri na mauwa yake ambayo ni karoti, njegere na hoho.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Namna bora ya kupamba nyumba msimu wa sikukuu





MSIMU wa sikukuu umewadia huku kukiwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba, kukiwa kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Kama kawaida, msimu huu unapowadia, huwa kunaonekana tofauti kutokana na mapambo au urembo unaopambwa sehemu mbalimbali iwe ofisini, nyumbani na maeneo mengine.

Katika kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, kuna sikuu za Krismasi na Mwaka Mpya ambazo kwa ujumla wake zote ni muhimu kwa uzito wake.

Katika makala hii ya nyumba, tunaweka dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitasaidia kuifanya sikukuu yako kuwa nzuri, ukaifurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba kipindi hiki familia nyingi huwa zinaungana pamoja katika mapumziko ya mwisho wa mwaka. Wazazi wengi wako likizo na watoto nao wamefunga shule, familia zimejumuika nyumbani kwa hiyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa ni cha furaha zaidi nyumbani.

Katika kipindi hiki, ni muhimu nyumba ikawa na vionjo tofauti hususani mapambo yenye kumbukumbu ya kifamilia ambayo pia yanachangia kuleta furaha katika kipindi hiki ambacho familia imejumuika pamoja nyumbani.

Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wall papers' na mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na sikukuu pamoja na maua ya kawaida au ukaweka kumbukumbu ya picha za pamoja za familia kama zipo.

Mapambo mengine ambayo unaweza kutengeneza ni ya maua ya asili kwa kuyaweka katika chombo au chupa maalum ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.


Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.

Pia unaweza kutengeneza maneno yenye ujumbe maalum kwa kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalum yanapopatikana na kuyaweka nyumbani kwako.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Pia nyumba katika msimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa musimu wa sikukuu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya mwonekano wa nyumba yako.




...KINYUNYIZO CHA LEO...

...UKURASA HUU UNAWATAKIA NYOTE SIKUKUU NJEMA YA KRIMASI....

## HABARI KIMATAIFA

# Zambia yafuta adhabu ya kifo

**LUSAKA,** ZAMBIA

SERIKALI ya Zambia imetangaza kufuta sheria inayotoa adhabu ya kifo, hatua ambayo imepongezwa na wanaharakati kuwa ni hatua muhimu katika kuheshimu haki za binadamu.

Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, ambaye chama chake kinachotawala sasa kimekuwa upande wa upinzani kwa miongo miwili, baada ya kuingia madarakani aliahidi kufuta sheria zote kandamizi ambazo zilikuwa zikilalamikiwa kuwa zinakiuka haki za binadamu.

"Rais Hakainde Hichilema ametia saini sheria ya mwenendo wa adhabu ya mwaka 2022 na kufuta adhabu ya kifo na kosa la jinai la kumkashfu Rais, ambazo zimekuwamo katika vitabu vya sheria tangu wakati wa ukoloni," msemaji wa Rais, Anthony Bwalya, alisema katika taarifa iliyotolewa juzi.



Hakainde Hichilema

Kutokana na kufutwa kwa sheria hizo, mwanaharakati wa haki za binadamu, Brebner Changala, alisema uamuzi huo ni hatua kubwa katika kuondokana na sheria kandamizi ambazo nyingi zilitungwa wakati wa ukoloni na zilikuwa zinaminya demokrasia na uhuru wa kujieleza.

Mkurugenzi Mtendaji wa asasi inayojishughulisha na masuala ya sera (CPD), Caroline Katotobwe, alisema kutokana na kufutwa kwa sheria hizo, wananchi wa Zambia sasa watakuwa na uhuru wa kuzungumza bila woga.

"Tukiwa wadau, tumefurahishwa kwamba sheria hizi kandamizi sasa tumeondokana nazo. Kwa maana hiyo, watakuwa huru kutoa mawazo yao kwa uhuru bila kuogopa kuwa watashtakiwa kama ilivyokuwa zamani," alisema. Zambia ilipata uhuru kutoka kwa wakoloni wa Kiingereza wakati huo ikiitwa Rhodesia ya Kaskazini. Kwa sasa taifa hilo linakadiriwa kuwa na watu milioni 18.

**– THE MONITOR.**



Magari na miundombinu mbalimbali vikiteketea baada ya majeshi ya Russia kushambulia mji wa Kherson, Ukraine, jana.
**PICHA: BBC**

# Makombora ya Russia yaua wanane Ukraine

**KIEV,** UKRAINE

MAJESHI ya Russia yamerusha makombora katikati mwa Kherson na kusababisha vifo vya watu wanane huku raia wengine 17 wakijeruhiwa.

Mashambulizi hayo, kwa mujibu wa ofisi ya mwendesha mashtaka wa Mkoa wa Kherson, yalifanywa jana asubuhi.

"Watu kadhaa wamelazwa hospitalini wakiwa na majeraha mabaya. Miundombinu ya kiraia imeharibiwa, ikiwa ni pamoja na majengo ya makazi, utawala na magari," ilieleza ripoti hiyo.

Mashambulizi hayo yamefanyika yakiwa ni mwendelezo wa ufyatuaji wa makombora unaofanywa na majeshi ya Russia. Hivi karibuni, kulikuwa na shambulio ambalo lilifanyika karibu na soko kuu siku ya soko.

"Russia imefanya shambulio lingine la kigaidi, wamerusha makombora katikati ya jiji. Watu wamefariki dunia, majengo yameharibiwa. Shambulizi limefanyika siku ya mapumziko, watu wengi walikuwa mitaani," alisema Naibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Kyrylo Tymoshenko.

Kutokana na shambulio hilo, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema kitendo hicho ni cha kigaidi.

"Nchi ya kigaidi inaendelea kurusha makombora kwa raia huko Kherson. Jumamosi asubuhi, siku ya kuamkia Krismasi, katikati mwa jiji kumeshambuliwa. Hii si miundombinu ya kijeshi. Hii si vita kwa mujibu wa sheria.

Huu ni ugaidi, haya ni mauaji kwa ajili ya kuongeza hofu na vitisho kwa raia. Dunia inatakiwa kuona na kuelewa ni uovu gani hasa tunapambana nao," aliandika Rais huyo katika ukurasa wake wa Twitter.

**BBC.**

# Mwanaharakati aibua unyanyasajiwa wanawake waliowekwa kizuizini

**TEHRAN,** IRAN

MWANAHARAKATI wa haki za binadamu nchini Iran, Narges Mohammed, ameandika akiwa gerezani kuhusu wanawake waliowekwa kizuizini kutokana na maandamano ya hivi karibuni, wanavyonyanyaswa kimwili na kingono.

Katika taarifa aliyoitoa kwenye vyombo vya habari vya kimataifa, likiwamo Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), mwanaharakati huyo alisema vitendo kama hivyo vimekuwa vya kawaida katika magereza na mahubusu.

Narges ambaye anatumikia kifungo cha muda mrefu katika gereza maarufu la Evin la Tehran, alizuiwa na polisi katikati ya Septemba, mwaka huu, kwa madai ya kuvaa hijabu yake, 'isivyofaa'.

Maandamano ya hivi karibuni, yalichochewa na kifo cha Mahsa Amini mwenye umri wa miaka 22, akiwa kizuizini baada ya kukamatwa kwa kukiuka kanuni kali za mavazi.

Kwa mujibu wa wanaharakati wa haki za binadamu, zaidi ya waandamanaji 500, wakiwemo watoto 69, wameuawa huku wengine maelfu wakikamatwa.

Inadaiwa kuwa waliokamatwa wengi wanateswa na kudhulumiwa huku wengine wakiendelea kupata shida vizuizini.

Narges ambaye ni Naibu Mkuu wa Kituo cha Watetezi wa Haki za Kibinadamu cha Shirin Ebadi na mshindi wa Tuzo ya Nobel amekuwa akihukumiwa vifungo mbalimbali jela tangu waka 2011 na hadi sasa yuko gerezani.

Licha ya tuzo ya Nobel, Narges pia mwaka huu alijumuishwa katika orodha ya BBC ya wanawake 100 wenye ushawishi kutoka duniani kote.

**– BBC.**

# Mkuu utumishi mstaafu afariki

**KAMPALA,** UGANDA

MKUU wa zamani wa Utumishi Serikali nchini Uganda, Dk. John Mitala, amefariki dunia, mmoja wa watu wa karibu wa familia hiyo amesema.

Baada ya kuwa katika utumishi wa umma kwa miaka 48, Septemba mwaka jana, Dk. Mitala alistaafu rasmi utumishi na kumwachia kijiti nafasi ya mkuu wa utumishi wa umma na katibu wa baraza la mawaziri Lucy Nakyobe, ambaye kabla ya kushika wadhifa huo, alikuwa Mnikulu.

Wakati wa kukabidhi kijiti, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu,

Milly Babalanda, alimpongeza Mitala kama mtu aliyetumikia kwa uaminifu na kwa namna ya kipekee katika utumishi wa umma.

Babalanda alisema tofauti na watumishi wengi, ambao hutafuta kazi katika utumishi wa umma kwa ajili ya manufaa binafsi, jina la Mitala halijawahi kuchomoza katika orodha ya vigogo waliokuwa wakishukiwa kujihusisha na rushwa.

"Utendaji wako uliotukuka utakumbukwa kwa muda mrefu katika utumishi wa umma nchini Uganda ma Jumuiya ya Afrika Mashariki. Umeonyesha viwango vya hali ya juu. Watu wengi wanaamini kwamba kufanya kazi katika utumishi wa umma Uganda, maana yake ni kujitajirisha au kujipatia fedha za haraka.

"Hata hivyo kwa muda ambao nimekufahamu (Mitala), sijawahi kusikia jina lako katika kahfa za rushwa," alisema Babalanda.

Mitala alijiunga na utumishi wa umma Mei 25, 1973 akifanya kazi katika Wizara ya Jinsia, Kazi na Maendeleo ya Jamii akiwa na umri wa miaka 19.

Baadaye alipanda cheo na kuwa naibu mkuu wa tume ya utumishi wa umma na tume ya utumishi wa mahakama hadi mwaka 2002 alipoteuliwa kuwa mkuu wa utumishi serikalini.

**– THER MONITOR.**

## SAFU

### MAKALA

# KANSA YA UONGOZI AFRIKA NI HII



Na Magabilo Masambu

RAIS wa Kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere aliyataja mambo manne kama msingi wa maendeleo. Ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Watu ni nguvu kazi ndiyo kusema tukiwa na watu wengi tunategemea maendeleo yatakwenda kasi kwa sababu tunategemea watafanya kazi kwa bidii ili kuzalisha zaidi mashambani na viwandani.

Tukiwa na siasa safi inapelekea kuwa na uongozi bora kwa sababu siasa ni mfumo ambao unatupatia viongozi. Tukiwa na ardhi ikatumika vizuri, maana yake itatupatia mali nyingi kama mazao na vilivyomo chini ya ardhi kama madini.

Karibu mambo yote hayo tunayo lakini tatizo ni namna gani tunaweza kuyatumia katika kujiletea maendeleo yetu. Watu tunao ni hivi karibuni tu tumeambiwa sasa tuko zaidi ya watu milioni 60 si haba. Ardhi tunayo kubwa na iliyotumika hasa katika uzalishaji ni asilimia ndogo sana. Siasa safi hatuwezi kujisifu sana na kama hatuna siasa safi maana yake kupata uongozi bora nacho kitakuwa kipengele kwa sababu uongozi bora ni zao la siasa safi.

Tatizo kubwa tulilo nalo Afrika kwa ujumla ambalo naliita ni kansa ya uongozi ni kuhusu baadhi ya viongozi kutoyaona makosa wanapokuwa na nafasi za madaraka. Kuna mtu mmoja mahali fulani aliwahi kusema viongozi wengi wa Afrika, huwa wanapata akili za uongozi pindi wanapoyaacha madaraka au kwa kustaafu au kutolewa kwenye nafasi. Yaani mtu akiwa nje ya nafasi ya uongozi, anakuwa mkosoaji na mshauri mzuri wa masuala ya uongozi lakini akiwa ndani, anakuwa hayaoni makosa.

Jambo hili nimewahi kumuuliza kiongozi mkubwa tu kwamba inakuwaje viongozi wakiwa kwenye madaraka wanashindwa kuyaona makosa mpaka wanapokaa pembeni? Akaniambia bwana mdogo tulifundishwa huko zamani kwamba wakati wa kula si vyema ukawa unaongea maana mdomo wakati huo unatumika kula na si kuongea maana watu wataona unachotafuna. Akanisisitiza kuwa si kwamba watu hawaoni makosa yanapotokea bali si busara wakati wa kula kutumia mdomo wako kuzungumza.

Imekuwa kawaida sasa kwamba watu walioko nje ya mfumo wa uongozi, wanaonekana kuwa wazuri na wenye kuona upungufu zaidi lakini inapotokea wakazipata nafasi zile, huwezi kuona mabadiliko makubwa. Jambo hili linapunguza matumaini na imani kwa watu juu ya walio nje ya mifumo ya kiuongozi kuaminika na kwamba pengine nao wakipata madaraka wembe utakuwa ule ule.

Nadhani tunapaswa kubadilika, tushauri na kukosoa kwa nia njema kabisa juu ya mambo makubwa yanayogusa maslahi ya taifa bila woga wa nini kitatokea. Kama tutakuwa na maono makubwa tukashauri vizuri, hata tukionekana wabaya leo, kesho ukweli utatutetea.

Hili jambo limekuwa sasa kama utamaduni. Kwamba tukitaka kupata madaraka makubwa zaidi ni kupiga kelele zaidi ili tutupiwe mifupa mara tukishaidaka tunahangaika kuitafuna huku mambo yakiharibika. Imefika mahali hata baadhi ya wabunge wakitaka kuwa mawaziri, wanapiga kelele sana si kwa sababu wanakerwa na yanayofanywa, hapana. Wanaona hiyo ni fursa ya kujipandisha zaidi na wakishazipata nafasi hizo, nao wanageuka kuwa watetezi wa yale waliyokuwa wakiyapigia kelele!

Ni kweli kwamba mfumo wowote ukishakuwa na waharifu wengi, wale wema wachache hugeuka kuwa maadui na ili kufanana nao, utalazimika na wewe kuwa kama wao. Utawala bora na uwajibikaji ni pamoja na kuachia nafasi unapoona mambo yanayofanyika si dhamira yako. Si kazi rahisi lakini kwa maslahi ya nchi na taifa ni muhimu lakini kabla ya kuachia unapaswa uwe umeshauri bila uoga kwamba, jamani nadhani huku tunakokwenda au hiki tunachokifanya kitarudisha maendeleo yetu nyuma zaidi nafikiri tungepita hapa. Badala yake tunangoja tukishazikosa nafasi hizo ndipo tunaanzisha ligi.

Kukosa uongozi bora ni pamoja na matumizi mabaya ya madaraka. Wale waliopewa madaraka na wananchi moja kwa moja au kupitia nafasi za uteuzi lazima wajue kwamba wamepata fursa hizo ili kustawisha maisha ya wengine na si maisha yao binafsi. Hatutapiga hatua za maendeleo kamwe ikiwa kila kiongozi kwa nafasi yake anawaza kupiga kila pesa inayopitia mikononi mwake.

Baadhi ya maeneo wawekezaji wanashindwa kuanzisha miradi kwa sababu yuko kiongozi mmoja tu anataka asilimia 10 vinginevyo mradi usifanyike. Wakati mwingine unajiuliza kwani hiyo miradi ni kwa ajili ya kina nani? Kama ni maendeleo yetu sote, tunawezaje kuwa na uwezo wa kuyazuia eti kwa sababu tunakosa chochote? Yaani ni sawa uko shimoni unatupiwa kamba utoke wewe unaikataa lakini huna uwezo wa kutoka humo bila ngazi.

Suala la kuwajibika na kuachia nafasi inapotokea kiongozi anatuhumiwa au kuthibitika ametenda makosa hasa ya matumizi mabaya ya fedha za umma nalo Afrika ni msamiati ambao umekosa majawabu. Wenzetu tuhuma ndogo tu zinamfanya awajibike. Tukiacha kutumia nafasi za uongozi kama sehemu ya kutengeneza maisha yetu binafsi. Tutafanikiwa kujiletea maendeleo sisi sote, maana tukijenga barabara tunazitumia wote. Tukijenga shule tunasoma sote kadhalika na huduma za afya. Tusisubiri kukosoa na kushauri tuwapo nje ya madaraka tufanye hivyo tungali tukiwamo.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmailcom**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

### BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Mjane aliyeonyeshwa njia mumewe alipofariki dunia*



Na Adam Fungamwango

NAKUMBUKA mwanzoni mwa miaka ya 2000, nilikuwa na rafiki yangu aliyekuwa anaishi maeneo ya Mwenge, Dar es Salaam, mwenye mke na mtoto mmoja wa kike. Alianza kuumwa, lakini ni kama alianza kuhisi kitu kisichokuwa cha kawaida.

Aliyekuwa akimhangaikia kwenye matibabu ni mkewe tu na kampuni aliyokuwa akifanyia kazi. Ndugu walionekana kuwa mbali naye kidogo.

Akamwambia mkewe kuwa kuna leo na kesho. Ugonjwa anaoumwa anaweza kupona au kutopona, hivyo akamshauri awe anatoa vitu kidogo kidogo ndani na kupeleka kwao.

Mke akashangaa, akataka kubisha akimwambia atapona tu asiwe na wasiwasi. Mume akamwambia kama akipona vitu vitarudi, lakini asipopona basi iwe mali yake.

Alipouliza, mume alimjibu kuwa alishaona mambo mengi kuhusu familia kadhaa hasa mume anapofariki na wanachofanyiwa baadhi ya wanawake.

Akamwambia yeye anawafahamu ndugu zake jinsi walivyo, anaweza asiambulie chochote.

Mke akakubali, akaanza kuondoa kitu kimoja kimoja, hasa vile ambavyo anaona ni vya muhimu na vya gharama na hati za nyumba na shamba.

Mwezi mmoja tu baadaye, rafiki yangu akafariki dunia. Kilichotokea kinashabihiana na kile alichosema. Ni kwamba walifumuka ndugu hata wengine hawajulikani walipotokea na hawajawahi kuonekana hata siku moja.

Walichofanya ni kuja na basi pamoja na lori ambalo lilitumika kupakiza samani za ndani na msiba ukapelekwa Dodoma na si pale tena.

Cha kushangaza baadhi ya ndugu wakaanza kumuuliza baadhi ya vitu ambavyo havionekani ndani. Mke akawajibu hati na vitu vingine hajui vilipo na hajawahi kuviona, lakini baadhi ya vitu vya ndani aliweka rehani ili apate pesa za kumtibia mumewe, hivyo kama wanavihitaji watoe fedha wakavigomboe. Wakashindwa.

Ikawa ndiyo afadhali yake yule mama. Vinginevyo, bila ushauri wa mumewe kabla hajafa angeambulia patupu.

Yuko mmoja aliyenyang'anywa ufunguo hospitalini baada ya mumewe kufariki. Anafariki tu hapo hapo, mke anaambiwa atoe ufunguo na asikanyage pale kwani hana chake tena.

Katikati ya miaka ya 1980 kuna mjane mmoja alipewa kinu, mchi, kibao cha mbuzi na vifaa vya jikoni tu, lakini vitu vyote walichukua ndugu wa marehemu.

Kwa sasa naona juhudi zinafanyika na akinamama wanaonekana kuelimishwa na kuelimika kudai haki zao hasa wanapofika hapo na yapo mashirika mbalimbali ya wanawake wanayowasaidia, hasa kisheria.

Hata hivyo bado msaada huu haujaweza kuwafikia wanawake wengi, hasa vijijini na sehemu zilizo mbali na huduma hizo, kwani wanaendelea kunyanyaswa. Na wapo ambao bado hawajajua waanze vipi au wafanye vipi kusaka haki zao.

Haya yalianza zamani sana na ndiyo maana DDC Mlimani Park Orchestra waliwahi kutunga wimbo uitwao 'Mnanionyesha Njia ya Kwetu', unaozungumzia sakata la ndugu wa marehemu kugawana mali, huku wakimtenga mke wa marehemu na watoto wake.

"Mnanionyesha njia ya kwetu, huku mkinisimanga sina changu tena, wala faida kwenu. Hata tanga bado halijaisha mnaanza kugawana mali ya marehemu mume wangu eee, ninapouliza yamekuwaje, jibu ni kwamba mnagawana mali ya mwanenu."

Mke anauliza imekuwaje? Mbona wanagawana mali ya mumewe, akajibiwa na wakwe zake huyo ni mtoto wao, yeye ni mke tu.

Mbali na hayo akaonyeshwa njia ya kwao. Aondoke na watoto wake, pale hapamhusu tena.

"Mbona mmesahau ya kuwa mali hiyo haswa, ni ya watoto na msimamizi ni mimi mama yao, ambaye leo mnanikana. Kama ni mila tuache, tuache kwa sababu madhara yake ni makubwa."

Mke anawashangaa wakwe zake na kuwaambia hiyo mali wanayogawana kisheria ni ya watoto na msimamizi ni yeye mama yao ambaye leo wanamkana. Anawapasha kuwa kama hiyo ndiyo mila yao waiache kwa sababu madhara yake huko mbele ni makubwa sana.

"Mlikuwa mkiniita mke ooo, wengine shemeji oo, wengine wifi oo, lakini hayo mmeyasahau kama ni msiba ni wa kwetu sote, kama ni msiba mama ni wa kwetu sote.

Madhara yake ni makubwa, madhara yake ni makubwa, wengine mliita shemeji oo, wengine mliita mimi wifi oo, wengine mliita shangazi ooo."

Mke analalamika kutengwa. Ndugu wote wa marehemu wanaonekana hawamtaki, kisa ni mali tu. Anawaambia siku zote walikuwa wakimwita mke, wengine shemeji, wifi, shangazi, lakini leo wameyasahau wanamuona kama mtu baki aliyejileta mwenyewe. Kisa ni kwa ajili ya mali tu?

Haya ni mambo ya kukemewa sana kwenye jamii yetu na yamepitwa na wakati. Kila mmoja ana wajibu wa kuliacha na kulikemea jambo hili ambalo linawachangaya na kuwarudisha nyuma sana akinamama. Wanaishi na wanaume kwa miaka zaidi ya 10, halafu ndugu bila sababu yoyote wanataka kuchukua mali na kumtimua akaanze upya.

Wimbo huu umetungwa na Cosmas Chidumule. Ninachoshangaa ni kwamba matatizo kama haya ya kijamii yanayowapata wanawake yanatakiwa kutungiwa na kuimbwa na wasanii kama kina Zuchu, Nandy na wengine. Lakini wao wanaimba mapenzi tu.

Kwenye mapenzi kuna mambo mengine ambayo yapo nyuma ya pazia. Kuna raha na karaha kama hizi. Wangekuwa nao wanaimba ili kuelimisha na kuonya jamii. Ona Chidumule ametunga wimbo miaka ya 1980 akiwawakilisha akinamama na hadi leo una maana kubwa na haupitwi na wakati na unapendwa. Kina Zuchu na Nandy wanakwama wapi?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.

# Harusi imevunjika-11

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele.

Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

****************************************




Kando ya mama yake Vayajo alikuwa amejaa tele kama pishi la mchele. Zulfa alimuona vizuri dada yake aliyekuwa amepeleka kidole chake mdomoni. Ilikuwa ni ishara aliyoifahamu vema. Ya kwamba afunge mdomo wake. Ina maana asimwambie lolote mama yao.

"Vipi mwenzetu mbona hivyo?"

Hakujibu kitu, alikwenda ndani kutua ndoo. Akabaki ndani kwa dakika 10 hivi. Alipotoka alikuwa amebadilisha nguo.

"Enhe mwenzetu kimekupata nini mbona hivyo?"

"Nilianguka." Akajibu kifupi kwa haraka.

"Wapi?" Mama akauliza tena.

"Njiani wakati narudi na maji, ikabidi nirudi tena nikachote." Akazidi kumdanganya mama yake.

"We nawe umezidi kutembea kama bata, ndiyo maana huwa unaangukaanguka."

Wakati huo pembeni, Vayajo alikuwa anakauka kwa kucheka, ingawa kimya kimya bila kutoa sauti.

Mama aligeuka ghafla kama kuna kitu alitaka kumwambia Vayajo. Alichokutaka nacho ni kicheko cha kimya kutoka kwake.

"Na wewe kinachokuchekesha nini? Mwenzako kaanguka wewe unacheka badala ya kumpa pole.

"Mimi nimecheka hilo neno la kuwa anatembea kama bata." Vayajo naye alidanganya.

*******************************

"Babu mi' nimekuja, maana hata sielewi."

**Ilikuwa rahisi kwa mwanamume kupishana naye akashindwa kugeuka. Iwe akikutana naye kwa mbele na lazima atageuka akishapitana naye, na hata kama atakuwa nyuma yake, akishampita tu atageuka kuangalia sura.**

"Nini mjukuu wangu mbona hivyo?"

"Maana babu wa kwanza kukwambia ni wewe, hata baba na mama sijawaambia hivyo!"

"Kuna nini tena Zulfa, mbona unanishtua?"

"Huyo mjukuu wako Vayajo, mimi simuelewi, yaani siku hizi ananichukia, ananiambia maneno ya ajabu ajabu, simuelewi"

"Kwani umemfanya nini dada yako?"

"Nimfanye nini mimi? Nashangaa tu tangu nirudi hapa, nimemkuta, ukimsalimia mara aitikie kwa tabu, mara anyamaze, juzi kanivizia natoka kisimani, babu wewe, hukuwepo malaika wako alikuwepo, 'nilichambwa', nilitukanwa, babu, unajua kutukanwa. Sikubakishwa hata unywele."

"Nyinyi watoto nyinyi!"

"Babu, nilitiwa singi, nikapigwa kikumbo nikaangukia kule, ndoo ya maji kwake, mimi kwangu."

Zulfa alikuwa akijaribu kumuelezea mambo yaliyomkuta siku chache tu baada ya kuwasili kutoka mjini.

Wakati mama Zulfa alikuwa kipenzi cha Vayajo, mzee Mbegu yeye alikuwa anampenda Zulfa.

Ndiyo maana Zulfa alikuwa akisitasita kumwambia mama yake kwani alijua yatakuwa makubwa na yanaweza kuwa magumu upande wake, hivyo na yeye alikwenda kumuelezea babu yake ambaye anajua ukimkata tu utamkuta yeye amejaa.

"Mimi ndiyo kipenzi chako, hebu nipe sababu ya wewe kugombana na dada yako."

"Najua basi babu, mara mimi najifanya mzuri, mara huniwezi, na anasema siku hizi ananichukia sana."

"Anakuchukia?"

"Ndiyo, hataki hata kuniona, sijui nimemfanya nini, kwani huku kijijini kulitokea nini babu?"

"Mmmh! Basi nimeshajua kwa nini anakuwashia moto."

"Unajua alipofika hapa wewe hukuwepo. Ulikuwa kwa Jerry. Na anajua umekaa huko kwa miezi miwili. Naona hana imani na wewe."

"Babu kweli hilo?"

"Mimi naona hivyo, sasa tatizo kama si hilo ni lipi?"

"Kama ni hilo basi da' Vayajo atakuwa ana matatizo. Mimi nilikaa kule siyo kwa kupenda. Nilikuwa naugua. Nimeuguzwa na kaka wa watu siyo ndugu yetu na yeye kamfanyia kituko cha mwaka, lakini kakubali kunichukua, kanipeleka hospitali matibabu yote amelipia yeye, nimekaa naye miezi miwili nyumbani kwake kaniuguza na kunitunza mtoto wa watu, yeye sijui alikuwa wapi huko..."

Akakatishwa na kicheko kutoka kwa babu yake.

"Sasa na wewe babu unacheka nini?"

"Si nilikwambia wewe, kubali akuchukue moja kwa moja kwa mahari ile ile ya dada yako ukakataa, haya sasa ndugu yako huyo huyo amekulisha nyama haramu, hujafanya chochote anakutuhumu, si bora angerudi na kukukuta umehamia tu huko huko tuone kama angekufuata?"

Ikabidi Zulfa naye aangue kicheko kwa maneno ya babu yake.

"Babu wewe ni mtu mzima, nakuamini, inawezekana, lakini ngoja na mimi nifanye uchunguzi wangu, kama ni kweli basi mbona dada atakuwa ananifikiria vibaya hivyo."

"Lakini yeye si alikimbia hapa kabla ya kuja kufungishwa ndoa, sasa wivu wa nini kwa mdogo wake?"

"Hapo sasa babu, ingekuwa amefunga ndoa kweli, au wameshawahi kuishi wote, lakini hata ndoa bado, katoroka, sasa leo ndiyo anamuona mzuri eeee, hehehe, amechelewa babu weeee." Akasema huku akijitingishatingisha kwa mbwembwe na mikogo kiasi cha kumvunja mbavu babu yake.

"Kwani dada yako anataka amuombe msamaha ili warudiane au vipi?"

"Najua basi, mradi wewe umeshanipa mwongozo kuwa kisa kitakuwa ni huyo aliyemkimbia mwenyewe au?"

"We unafikiri Jerry atakubali kwa aibu ile aliyompa?"

"Mhh, babu huwezi kujua, mapenzi haya, huwezi kujua mtu rohoni mwake."

"Wewe si umeishi naye miezi miwili huko Dar, alikuwa anaonekanaje? Anamtajataja au?"

"Babu nikwambie tu ukweli, mimi nimekaa naye hata kumtaja tu alikuwa hamtaji. Kuna wakati mimi nilikuwa najisahau namtaja. Kwa sura tu alikuwa anaonekana kama anachukia, ingawa hata siku moja hajawahi kuniambia hapendi nimtaje, lakini alionekana kabisa anakuwa kama hataki hivi, na mimi nikabadilika nikawa sisemi lolote kuhusu da' Vayajo."

**INAENDELEA JUMAPILI**



# DIAMOND HUTOKI NA ZUCHU? AAA TUACHE BWANA

STAA wa muziki wa bongo fleva nchini Diamond Platnumz amefyatua ngoma tata kuelekea mwisho wa mwaka ambayo imeanza kuwa gumzo si kutokana na mirindimo na uimbaji wake, bali maneno yake yaliyowashangaza wengi kuwa hajawahi kuwa na uhusiano wa kimapenzi na msanii Zuchu.

Ngoma hiyo inaitwa 'Chitaki' ambayo ameiweka kwenye mtandao wa 'you tube', na instagram Desemba 23 na mpaka sana Desemba 24 tayari ilikuwa imeangaliwa na watu 366,561.

Hapana shaka kitakuwa ndiyo kibao cha kufungia mwaka 2022, na tayari alichokiimba kwenye ngoma hiyo kimeanza kuwa gumzo, kwani kwa muda wote huu mashabiki wake na wale wa muziki wa bongo fleva wanajua kuwa Diamond na Zuchu, japo wapo kwenye lebo moja na mtu na bosi wake, lakini wapo kwenye mahusiano ya kimapenzi kiasi kwamba kuna wakati ilisemekana wanakaribia kuoana.

"We ndiyo kitumbua, we ndiyo sambusa, basi njoo unichumu baby au ndiyo tuseme umesusa, we ndiyo mwisho wa reli kwako nimeweka nukta, waliokwambia nala Zuchu siyo kweli wanazusha. Waliokaa vikao sisi kutujadili, wape pole hao wanatwanga maji na waongeze bidii kwenye urogaji, tuko ten GB penzi full chaji..." Ni baadhi ya maneno yaliyo kwenye ngoma ya mkali hiyo.

Maneno hayo yamewaacha njia panda mashabiki wengi kiasi kwamba hawaamini kama ni kweli, na wengine wanadhani labda Diamond ametengeneza shairi hilo kwa ajili ya kupata vina, au kuzua mjadala kwenye mitandao na vijiweni ili 'kuibusti' ngoma yake.

Kwa muda mrefu sasa Diamond na Zuchu wamekuwa wakionekana pamoja, wakati mwingine kwenye mikao na matembezi ambayo yalikuwa yakiashiria kuwa wana uhusiano wa kimapenzi ingawa wenyewe huwa hawakatai wala kukubali kama ni mtu na mpenzi wake.

## ZISIKUPITE

### CITY YAMPANIA BELLINGHAM

MANCHESTER City imepania kushinda vita dhidi ya Borussia Dortmund ya kumsajili Jude Bellingham na inaamini kiungo huyo wa England mwenye miaka 19, atapata ofa ya pauni milioni 100 za uhamisho kwenda Real Madrid ama Liverpool na kufanya kazi na Kocha wa City, Pep Guardiola. ***(Sun)***

### GAKPO, UNITED WATETA

MANCHESTER United imefungua mazungumzo na PSV Eindhoven, kuhusu uwezekano wa kumsajili winga Mholanzi Cody Gakpo, 23. ***(Mirror)***

### RONALDO ANUKIA AL-NASSR

AL-NASSR ina matumaini itakamilisha usajili wa mshambuliaji Mreno aliyepo huru Cristiano Ronaldo, 37, kabla ya dirisha la Januari kufunguliwa. ***(CBS Sports)***

### DE JONG AWEKEWA NGUMU

KLABU ya Manchester United inaamini hatimaye inayo nafasi ya kumsajili Frenkie de Jong katika dirisha la majira ya joto, lakini inahisi Barcelona inajaribu kuongeza thamani yake kwa kusema kiungo Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 25, hauzwi. ***(Sport - in Spanish)***

### NEWCASTLE KWA THURAM

NEWCASTLE inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Marcus Thuram, 25. ***(Times)***

### PSG YAMTAKA FRED

PSG pia inamhitaji kiungo wa Brazil na Manchester United, Fred, licha ya miamba hiyo ya kutaka kumuongeza miezi 12, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sun)***

### FOFANA AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA inakaribia kukamilisha dili na mshambuliaji wa Molde na Ivory Coast, David Datro Fofana, 20, pamoja na kiungo wa Vasco da Gama, Mbrazil Andrey Santos, 18. ***(Standard)***

### ARSENAL KINARA KWA FELIX

ARSENAL inaongoza mbio na Manchester United kumsajili mshambuliaji Mreno, Joao Felix, 23, kwa mkopo kutoka Atletico Madrid mwezi ujao. ***(Daily Record)***

### MILAN YAPANIA KWA LEAO

AC Milan inajiandaa kukutana na Rafael Leao, ambaye mkataba wake unamalizika 2024, na kumpa ofa ya mshahara mara tano zaidi ya anaolipwa kwa sasa. Mimba hiyo ya Italia inataka kumfanya Mreno huyo mwenye umri wa miaka 23, kuwa mchezaji anayelipwa zaidi ili kumvutia. ***(Corriere della Sera, via AS)***

### KESSIE, BELLERIN, HAWAUZWI

BARCELONA haina nia ya kumuuza kiungo raia wa Ivory Coast, Franck Kessie, 26, ama beki wa kulia Mhispania Hector Bellerin, 27, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA KUIKOSA SAINI YA GUNDOGAN CITY

**BARCELONA,** Hispania

●●● Kocha Guardiola anaona kiungo huyo mwenye mabao 51, anaweza kuwa muhimu kwao...

BARCELONA inaweza kuikosa nafasi ya kumsajili kiungo inayemwinda, Ilkay Gundogan, kwa mujibu wa Football Espana.

**Taarifa hizo zimedai kuwa nyota huyo wa kimataifa wa Ujerumani anajiandaa kusaini mkataba mpya na Manchester City ambao utadumu hadi mwaka 2025. Kiungo huyo wa zamani wa Borussia Dortmund, mkataba wake wa sasa na miamba hiyo ya Etihad unamalizika majira ya joto ya 2023 na amekuwa akihusishwa sana kuondoka kama mchezaji huru.**

Uwezekano wa Gundogan kupatikana bure, kumeivutia Barcelona, ambayo imeingia sokoni kwa miguu yote miwili ikitaka kuboresha kikosi chake. Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola inaaminika kuwa bado anahitaji huduma ya nahodha huyo kwa siku zijazo na mazungumzo yanapangwa kuanza mwakani.

Mtaalamu wa usajili, Nicolo Schira, amethibitisha kuwa City wanaamini wanaweza kumbakisha Gundogan hadi mwaka 2025. Guardiola anaona kama mlengwa wa Barcelona, mchezaji wake huyo anaweza kuwa muhimu kwao wanapotafuta taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA.

Hivi karibuni, Barcelona imekuwa ikihusishwa na baadhi ya majina makubwa katika nafasi ya kiungo ambao wanaweza kupatikana kwa bei ya chini ama huru. 'Blaugrana' hao wanaonekana kuwa mbioni kumpoteza Sergio Busquets wakati huu mkataba wake ukimalizika majira ya joto. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia amekuwa akipigiwa upatu wa kujiunga na Ligi Kuu ya Marekani (MLS), katika Klabu ya Inter Miami.

Wakati huo huo, tangu alipoondoka Borussia Dortmund mwaka 2016, Gundogan amezidi kuimarika pale Etihad. Hisa zake zimeongezeka kwa kiasi kikubwa katika misimu michache iliyopita, na alibeba jukumu muhimu kwa kuisaidia City kushinda ubingwa wa Ligi Kuu England msimu uliopita.

Gundogan ameichezea City mechi 274 akifunga mabao 51 na kuchangia mengine 35 kwa kutoa pasi za mwisho ('assists').

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,059,8

JACKPOT
MECHI WIKI HII

TAREHE: 28,29 NA 30 DISEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/12/22 | 17:00 | Troyes vs Nantes | 2.34 | 3.48 | 2.78 |
| 02. 28/12/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Kasimpasa | 2.78 | 3.53 | 2.31 |
| 03. 28/12/22 | 22:00 | Portimonense vs Casa Pia Atletico | 2.36 | 3.14 | 2.99 |
| 04. 28/12/22 | 22:45 | St Johnstone vs Hearts | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 28/12/22 | 22:45 | Livingston vs St Mirren | 2.32 | 3.38 | 2.88 |
| 06. 29/12/22 | 17:00 | Giresunspor vs Gaziantep BB | 2.47 | 3.34 | 2.69 |
| 07. 29/12/22 | 19:00 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.36 | 3.15 | 3.05 |
| 08. 29/12/22 | 21:15 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 29/12/22 | 22:00 | GD Estoril vs Boavista | 2.27 | 3.13 | 3.18 |
| 10. 29/12/22 | 22:45 | Blackburn vs Middlesbrough | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 11. 29/12/22 | 22:45 | Wigan vs Sunderland | 2.69 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 29/12/22 | 23:00 | Nice vs Lens | 3.14 | 2.89 | 2.43 |
| 13. 30/12/22 | 11:45 | Western United vs Brisbane Roar | 2.49 | 3.24 | 2.74 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KROOS KUAMUA FEBRUARI REAL MADRID



**MADRID,** Hispania

TONI Kroos ataamua mustakabali wake wa baadaye hapo Real Madrid, ifikapo Februari mwakani, kwa mujibu wa gazeti la MARCA.

Kiungo huyo wa kimataifa wa Ujerumani yupo katika mwaka wake wa mwisho wa mkataba na miamba hiyo ya Santiago Bernabeu na kuna uwezekano wa yeye kutundika daluga mwaka ujao. Kinyume chake pia anaweza kusaini mwaka mmoja na klabu hiyo.

'Los Blancos' hao watahitaji kwanza kusikia uamuzi kutoka kwa kiungo huyo wa zamani wa Bayern Munich ifikapo Februari, kitu ambacho kitawapa muda wa kuandaa mpango wao wa msimu wa 2023-24. Pia, amedai kwamba haoni mustakabali wake wa baadaye kwingineko.

Mapema mwaka huu, Kroos alisema: "Sijui hata nini kitatokea kuhusu mustakabali wangu wa baadaye, lakini ninauhakika sitacheza klabu nyingine."

Kroos atafikisha miaka 33 Januari mwakani, lakini ameendelea kuwa sehemu muhimu ya kikosi cha mfumo wa Kocha Carlo Ancelotti. Amefunga mara moja na kutoa pasi za mwisho 'assists' nne katika mechi 18 za mashindano kwa miamba hiyo ya Hispania msimu huu.



# Emery kuteta na Martine kumdhihaki Mbappe

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Aston Villa, Unai Emery, amepanga kuzungumza na kipa wake, Emiliano Martinez, kuhusu aina yake ya ushangiliaji baada ya kushinda Kombe la Dunia na Argentina.

Martinez amekuwa akikosolewa kuhusu baadhi ya vitendo vyake vya ushangiliaji baada ya mchezo wa fainali Jumapili iliyopita, ambayo ni pamoja na ishara mbaya na jeuri ya tuzo yake ya Golden Glove.

Pia, alimdhihaki mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe.

"Unapokuwa na hisia kubwa, wakati mwingine ni ngumu kuidhibiti," alisema Emery.

"Nitazungumza naye wiki ijayo kuhusu baadhi ya vitendo vyake vya ushangiliaji, lakini ninaheshimu kuwa sasa yuko chini ya timu ya taifa na atakapokuwa nasi, yeye ni jukumu letu basi tunaweza kulizungumzia.

"Tu wenye fahari sana kwake. Ameshinda Kombe la Dunia na timu yake ya taifa na inashangaza."

Argentina iliifunga Ufaransa mikwaju ya penalti 4-2 nchini Q baada ya fainali ya kuvutia kumali kwa sare ya mabao 3-3.

Wakiwa katika chumba cha kub ishia nguo baada ya mechi, Mart alitoa wito wa ukimya wa dakika n kwa Mbappe, ambaye alifunga trick kwa Ufaransa. Kisha akajihus katika dhihaka zaidi wakati wa g ride la ushindi la Argentina huko nos Aires, kwa kuinua mwanase anayeonyesha mshambuliaji huyo

Alhamisi, Noel Le Graet, rais Shirikisho la Soka la Ufaransa, iambia gazeti la kila siku la U ansa, Ouest-France, alikuwa am wandikia mwenzake wa Argen kuhusu sherehe "zisizo za kawa za timu.

Mambo ya Martinez wakati wa waju ya penalti yalipamba vichwa habari baada ya mchezo wa fai huku akili yake ikisumbua wach wa Ufaransa - akiokoa mkwaju penalti wa Kingsley Coman, na A lien Tchouameni akakosa.

344,733/-



# MPOLE APISHANA NA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA za zamani wa Geita Gold, George Mpole, amekaribishwa kwenye timu yake mpya ya FC Saint Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, lakini hatocheza michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika akiwa na timu yake hiyo mpya kutokana na jina lake kuwa kwenye orodha ya wachezaji wa timu yake ya awali aliyoicheza kwenye michuano hiyo hatua za awali.

**Kwa maana hiyo mchezaji huyo hatocheza mechi yoyote ya michuano hiyo wakati timu yake ikiwa kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, huku pia Yanga ikiwamo.**

Hata ikitokea FC Lupopo ikikutana na Yanga kwenye hatua yoyote baada ya makundi, Mpole hawezi kuwa sehemu ya kikosi kitakachocheza dhidi yao.

Mpole amekaribishwa kwenye klabu yake hiyo mpya, huku mtandao rasmi wa klabu hiyo jana ukichapicha picha yake ukimkaribisha kwa lugha ya Kifaransa, na mwisho neno la kiswahili 'karibu.'

Mbali na jina lake kusajiliwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, lakini pia alicheza mechi ya marudiano ya kombe hilo hatua za awali, Geita Gold ikiwa mwenyeji wa Hilal Alsahil ya Sudan, Septemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, ikishinda mabao 2-1.

Mpole hakucheza kwenye mechi ya kwanza ugenini, Geita Gold ikichapwa bao 1-0, ambapo ukiunganisha na matokeo ya mechi ya marudiano, timu hiyo inayomilikiwa na Halmashauri ya Mji wa Geita, iliondolewa kwa faida ya bao la ugenini baada ya matokeo ya jumla kuwa 2-2.

Kanuni za michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hairuhusu mchezaji mmoja kuchezea klabu mbili kwa msimu mmoja kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, hivyo kucheza michuano hiyo inabidi asubiri msimu ujao. Wakati Yanga iko Kundi D, Lupopo iko Kundi A.

Akizungumzia furaha yake ya kujiunga na timu hiyo, Mpole ambaye alikuwa mfungaji bora msimu uliopita akiwa na mabao 17, dhidi ya Fiston Mayele aliyemaliza na mabao 16, alisema atakuwa balozi mzuri wa Tanzania nje ya nchi.

## Saido aongeza makali Simba

INATOKA UK. 24

shatua Mwanza kujiunga na kikosi kinachojiandaa na mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya KMC, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza. Karibu mpambanaji wa kweli, fundi ambaye uwezo wake ni wa kipekee sana."

Akiwa kwenye klabu ya Yanga msimu uliopita alifunga mabao saba na kuiwezesha timu hiyo kutwaa ubingwa mara ya kwanza baada ya misimu minne.

Mchezaji huyo alisajiliwa na Yanga Oktoba mwaka 2020 akitokea Vital'O ya Burundi na kuitumikia kwa kipindi chote hadi aliposimamishwa na klabu yake kwa utovu wa nidhamu, lakini hapo hapo mkataba wake ulikuwa unafikia ukingoni, hivyo kuachana rasmi Mei mwaka huu.

Kulikuwa na taarifa za kusajiliwa na Simba, lakini aliibukia Geita Gold mwanzoni mwa msimu huu kwa mkataba wa mwaka mmoja.

Taarifa zinadai kuwa alishindwa kujiunga na timu hiyo mwanzoni mwa msimu akitoa Geita Gold baada ya wajumbe wa Bodi ya Simba kugawanyika kuhusu usajili wake.

## Fei Toto achafua hewa



INATOKA UK. 24

vizuri kwa ajili ya kutafuta pointi tatu muhimu," alisema Kaze.

Mwakilishi wa wachezaji, Dickson Job, alisema wamejiandaa vizuri na wanafahamu ubora wa Azam FC na wamepewa majukumu na kazi kubwa iliyobaki ni wao kwenda kufanya yale waliyopewa mazoezini.

"Tunawaheshimu Azam FC, wana timu nzuri na tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapambana kusaka alama muhimu ili kuendelea kuwa na tofauti kubwa ya pointi," alisema Job.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, John Matambala, alisema wamejipanga vizuri na wachezaji wako tayari kwa ajili ya mchezo wao dhidi ya Yanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Alisema mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa na kulingana na ukubwa wa mechi hiyo, kila moja itacheza kwa presha kwa sababu kila timu inahitaji matokeo ili kufikia malengo ya pointi tatu.

"Tunaingia na mbinu mpya tunaenda kucheza mchezo tofauti na mechi zilizopita kwa sababu ya kuhakikisha tunapata pointi muhimu na tunatambua ubora wa Yanga," alisema.

Mwakilishi wa wachezaji wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda, alisema mchezo huu ni mkubwa na kila mchezaji anapenda kucheza mechi hizi kubwa, hivyo wamejipanga kupata pointi tatu muhimu ambazo zitawaweka katika nafasi nzuri ya vita vya ubingwa.

"Tunatambua safu ya ushambuliaji ni nzuri, tumejiandaa kucheza na kuwazuia wachezaji wote wa Yanga na hatuchezi na Mayele (Fiston) pekee, tunahitaji kupata pointi tatu na tunaenda kuonyesha jambo ," alisema Mwaikenda.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/22 | 18:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.31 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/12/22 | 18:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 03. 26/12/22 | 18:00 | Rotherham United vs Stoke City | 2.90 | 3.25 | 2.40 |
| 04. 26/12/22 | 18:00 | Burton Albion vs Lincoln City | 2.37 | 3.30 | 2.90 |
| 05. 26/12/22 | 18:00 | Cambridge United vs Shrewsbury Town | 2.60 | 3.25 | 2.65 |
| 06. 26/12/22 | 18:00 | Charlton Athletic vs Peterborough United | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 26/12/22 | 18:00 | Exeter City vs Portsmouth FC | 2.65 | 3.35 | 2.55 |
| 08. 26/12/22 | 19:00 | FC Annecy vs AS Saint-Etienne | 2.90 | 3.25 | 2.37 |
| 09. 26/12/22 | 20:00 | Goztepe Izmir vs BB Bodrumspor | 2.50 | 3.35 | 2.65 |
| 10. 26/12/22 | 20:15 | Cardiff City vs Queens Park Rangers | 2.48 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 26/12/22 | 22:45 | Royal Charleroi SC vs RSC Anderlecht | 2.80 | 3.45 | 2.38 |
| 12. 26/12/22 | 22:45 | Luton Town vs Norwich City | 2.75 | 3.30 | 2.50 |
| 13. 26/12/22 | 23:00 | Valenciennes FC vs Amiens SC | 2.46 | 3.20 | 2.85 |
| 14. 26/12/22 | 23:00 | Pau FC vs Paris FC | 2.95 | 3.20 | 2.38 |
| 15. 26/12/22 | 23:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs Grenoble Foot | 2.46 | 3.05 | 2.95 |
| 16. 26/12/22 | 23:00 | SC Bastia vs SM Caen | 3.05 | 3.10 | 2.38 |
| 17. 26/12/22 | 23:00 | Nimes Olympique vs EA Guingamp | 2.90 | 3.25 | 2.40 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 25/12/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 1286 | Shams Azar Qazvin vs Arman Gohar Sirjan | 1.79 | 3.25 | 4.90 |
| 13:30 | 1626 | Chooka Talesh FC vs Khalijfars Mahshahr | 2.50 | 2.75 | 3.30 |
| 13:30 | 1771 | Teraktor Sazi vs Sanat Mes Kerman FC | 1.98 | 2.72 | 4.38 |
| 13:30 | 2002 | Adana Demirspor vs Fatih Karagumruk | 1.70 | 3.78 | 4.48 |
| 13:30 | 2422 | Kheybar Khorramabad FC vs Shahrdari Astara | 1.50 | 3.55 | 6.62 |
| 13:30 | 2476 | Mes Shahr-e Babak vs Darya Babol | 1.72 | 3.35 | 5.20 |
| 13:30 | 2547 | Boluspor vs Erzurum BB | 1.95 | 3.36 | 3.46 |
| 13:30 | 3607 | Vanpars vs Esteghlal Mollasani | 2.19 | 2.90 | 3.70 |
| 13:30 | 3809 | Pars Jonoubi Jam vs Fajr Sepasi | 2.01 | 3.00 | 4.20 |
| 13:30 | 4097 | Saipa Karadj vs Shahrdari Hamedan | 1.85 | 2.97 | 4.48 |
| 13:30 | 4493 | Keciorengucu vs Eyupspor | 2.83 | 3.27 | 2.27 |
| 13:30 | 4758 | Esteghlal Khuzestan vs Khosheh Talaei | 2.31 | 2.67 | 3.40 |
| 14:00 | 1431 | Zira vs Kapaz | 1.61 | 4.00 | 5.00 |
| 15:00 | 1233 | Persepolis FC vs Peykan FC | 1.49 | 3.80 | 7.40 |
| 15:45 | 2155 | Ahli Al-Fujirah vs Masafi | 2.47 | 4.10 | 2.39 |
| 15:45 | 2616 | Ismaily SC vs Al Masry Club | 2.63 | 2.53 | 3.33 |
| 15:45 | 3039 | Hatta Club vs AL Arabi | 1.75 | 4.08 | 3.54 |
| 15:45 | 3874 | AL Wahda Scc (UAE) vs Ajman Club | 1.52 | 4.09 | 5.06 |
| 15:45 | 4284 | Dibba Al Fujairah vs Al Sharjah SC | 8.38 | 5.07 | 1.28 |
| 15:45 | 4974 | Emirates Club vs Al-Thaid | 1.56 | 4.28 | 4.47 |
| 15:50 | 5875 | Gulf FC vs Masfoot Sports Club | 2.32 | 4.08 | 2.36 |
| 16:00 | 1063 | Mbeya City vs Tanzania Prisons | 2.25 | 2.90 | 3.50 |
| 16:00 | 1462 | Konyaspor vs Alanyaspor | 1.80 | 3.64 | 4.09 |
| 16:00 | 3869 | Club S Hammam vs Lif-EM Mahdia | 1.28 | 5.00 | 11.00 |
| 16:00 | 4518 | Genclerbirligi vs Bandirmaspor | 3.45 | 3.45 | 1.92 |
| 16:00 | 4708 | SS Sfaxien vs SC Moknine | 1.72 | 3.35 | 5.20 |
| 16:00 | 4719 | Gaziantep BB vs Besiktas | 3.63 | 3.78 | 1.87 |
| 17:30 | 2320 | Sanat Naft Abadan vs Esteghlal Tehran | 5.46 | 3.12 | 1.68 |
| 18:00 | 3490 | Arab Contractors vs Zamalek | 6.35 | 3.62 | 1.56 |
| 18:15 | 5527 | Kagera Sugar vs Geita Gold FC | 2.26 | 2.86 | 3.25 |
| 18:30 | 4378 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs Baniyas | 1.41 | 4.57 | 5.83 |
| 18:30 | 5343 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Ittihad Kalba | 2.29 | 3.45 | 2.67 |
| 19:00 | 2653 | Galatasaray vs Istanbulspor | 1.25 | 5.80 | 9.80 |
| 19:00 | 3633 | Samsunspor vs Adanaspor | 1.52 | 4.09 | 5.06 |
| 20:00 | 3963 | Al Ahly Cairo vs Smouha Club | 1.29 | 5.16 | 9.52 |
| 20:15 | 2578 | Azam vs Young Africans | 3.11 | 2.92 | 2.29 |
| 21:15 | 4583 | Bnei Sakhnin vs Hapoel Tel Aviv | 2.53 | 3.22 | 2.53 |

## JUMATATU - 26/12/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 1240 | Sunderland vs Blackburn | 2.30 | 3.17 | 3.03 |
| 15:30 | 5570 | Brentford vs Tottenham | 3.62 | 3.57 | 1.91 |
| 18:00 | 1038 | Crystal Palace vs Fulham | 2.02 | 3.43 | 3.43 |
| 18:00 | 1411 | Everton vs Wolverhampton | 2.26 | 3.16 | 3.11 |
| 18:00 | 1557 | Middlesbrough vs Wigan | 1.64 | 3.62 | 5.16 |
| 18:00 | 1755 | Sheffield Utd vs Coventry | 1.67 | 3.70 | 4.74 |
| 18:00 | 2870 | Southampton vs Brighton | 3.21 | 3.41 | 2.10 |
| 18:00 | 2936 | Rotherham vs Stoke City | 2.97 | 3.26 | 2.29 |
| 18:00 | 5466 | Leicester vs Newcastle | 3.12 | 3.37 | 2.16 |
| 18:15 | 1813 | KMC vs Simba | 5.16 | 3.66 | 1.26 |
| 20:30 | 2709 | Aston Villa vs Liverpool | 4.26 | 3.87 | 1.70 |
| 23:00 | 1629 | Arsenal vs West Ham | 1.54 | 3.94 | 5.63 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Desemba 25, 2022

Nipashe




Diamond hutoki na Zuchu? Aaa tuache

UKURASA 20

# Fei Toto achafua hewa Yanga, Azam

●●● Ni wakati zikivaana leo, sababu za kurudisha milioni 112 zaanikwa...

**Na Saada Akida**

WAKATI Azam FC ikiikaribisha Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam leo, kiungo fundi wa mabingwa watetezi hao, Feisal Salum 'Fei Toto', amechafua anga dhidi ya miamba hiyo baada ya kugeuka gumzo kwa hatua yake ya kudaiwa kuandika barua ya kuvunja mkataba wa kuitumikia klabu hiyo.

**Fei Toto ambaye hadi sasa katika Ligi Kuu msimu huu amehusika katika mabao nane ndani ya klabu hiyo akifunga sita na kutoa pasi za mwisho mbili, amekuwa msaada mkubwa ndani ya Yanga huku akifunga mabao muhimu wakati timu hiyo ikisaka ushindi.**

Ingawa bado haijatangazwa rasmi, inadaiwa Fei Toto amepata ofa nono zaidi ya kujiunga na Azam FC, na hivyo kutumia kipengele katika mkataba wake kinachomtaka kulipa Yanga Sh. milioni 100 kama akitaka kuvunja mkataba wake pamoja kuilipa mshahara wa mienzi mitatu, jambo ambalo alilitekeleza katika baraua yake ambayo Nipashe iliiona nakala yake.

Katika barua hiyo kwa Yanga inaeleza tayari ameilipa kiasi cha Sh. milioni 112, ambapo milioni 12 ni mishahara yake ya miezi mitatu, na zilizosalia ni ada ya kuvunja mkataba, hivyo kuwa mchezaji huru anayeweza kusajiliwa na klabu yoyote ile apendayo.

Moja ya chanzo chetu kilichopo karibu na mchezaji huyo, kililiambia Nipashe kuwa sababu zilizomfanya Fei Toto kufikia uamuzi wa kuvunja mkataba ni kutokana na kutosikilizwa ombi lake la kuongezwa mshahara kutokana na uwezo wake uwanjani.

Lakini pia akikerwa na mishahara mikubwa wanaolipwa baadhi ya nyota wa kigeni ambao anawazidi uwezo uwanjani huku baadhi yao wakisugua benchi.

"Fei Toto atakuwa amewafungulia njia wachezaji wazawa kutambua thamani yao uwanjani, mara nyingi wazawa wanalipwa kidogo kuliko 'mapro' (wageni) ambao wengine wanawazidi uwezo, hapa Yanga itabidi ijilaumu yenyewe, maana alitoa ombi lake la kuongezwa mshahara muda mrefu lakini hawakumjali," kilieleza chanzo chetu.

Licha ya kutoelezwa ni wapi anakwenda, lakini taarifa zinadai Azam FC imeweka mezani mshahara Sh. milioni 17 kwa mwezi huku ikiwa tayari kumjengea nyumba ya kisasa kwao Zanzibar pamoja na maslahi mengine mazuri.

Azam na Yanga zinavaana leo, mabingwa watetezi hao wakiwa kileleni na alama 44 na mabao 33 yakufunga na nane ya kufungwa wakati wenyeji wao, wana pointi 37, moja nyuma ya Simba iliyopo nafasi ya pili.

Kadhalika, safu ya ushambuliaji na ya ulinzi ya Azam inaonyesha kutokuwa na makali na uimara kama ilivyo kwa Yanga, kwani yenyewe imecheka na nyavu mara 25 na mabeki wakiruhusu mabao 16.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, asema utakuwa na utofauti na mzunguko wa kwanza kwa sababu ya muunganiko wa timu yao.

Alisema kikubwa wanahitaji kupata pointi tatu ili kuwapo na tofauti kubwa ya pointi kati ya Yanga na Azam FC katika vita vyao vya kupigania ubingwa.

"Tumejiandaa vizuri na kutakuwa na mabadiliko madogo na Bernard Morrison amefanya mazoezi na huenda akawapo katika kikosi cha kesho (leo), Azam wanakasi, viungo wako vizuri pamoja na benchi lao liko vizuri, lakini tumejipanga

INAENDELEA UK. 23



# Saido aongeza makali Simba

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imefanikiwa kuongeza makali katika kikosi chake baada ya kumsajili rasmi kiungo mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Mrundi Saido Ntibazonkiza kwa mkataba wa mwaka mmoja na nusu.

Saido amejiunga na klabu hiyo akitokea Geita Gold ambako aliichezea kwa nusu msimu ambapo tayari alikuwa ameshaifungia mabao manne na pasi sita za mwisho 'assists'.

Klabu ya Simba imesema tayari mchezaji huyo ameshawasili jijiji Mwanza kujiunga na wenzake ambao wanajiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumatatu dhidi ya KMC.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', amesema jana kuwa safari hii watafanya usajili makini bila shinikizo kutoka mahala popote.

Saido anakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa Simba kipindi hiki cha dirisha dogo, ambacho wanasaka wachezaji kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao.

Ikimtangaza rasmi jana mchezaji huyo kwenye mitandao yake mbalimbali ya kijamii, klabu hiyo imesema kwa uzoefu aliokuwa nao inaamini ataongeza ubunifu kwenye safu ya ushambuliaji akishirikiana na wachezaji waliopo.

"Klabu ya Simba inatangaza kufikia makubaliano na kiungo mshambuliaji Saido Ntibazonkiza kutoka Geita Gold kwa mkataba wa mwaka mmoja na nusu.

"Ntibazokiza, raia wa Burundi ni mchezaji mwenye uzoefu akiwa amecheza ligi za kimataifa mbalimbali, ikiwamo Ufaransa, Uturuki na Poland na hapa nyumbani ameshacheza ligi ya Tanzania kwa zaidi ya msimu miwili akiwa na timu kadhaa," ilisema na kuongeza;

"Kwa uzoefu wa Ntibazonkiza tunaamini ataongeza ubunifu katika safu yetu ya ushambuliaji, akishirikaiana na wachezaji waliopo. Katika msimu huu ameifuinga mabao manne na 'assists' sita katika timu aliyokuwa akiichezea ya Geita Gold.

"Tayari mchezaji ame-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >